# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Agosti 8, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580666





UKURASA 9

**SERIKALI** yafunguka kiini cha ongezeko la vifo Mkoa wa Kilimanjaro UKURASA 2



**ZIMEBAMBA MITAANI** Nywele za asili zinavyong'arisha warembo UKURASA 14

# Katoliki watoa waraka corona

UKURASA 3



## RIPOTI MAALUM:

## Ugoro, tumbaku janga lingine kwa afya nchini

UK. 4

## UKWELI KUHUSU CHANJO CORONA, NGUVU ZA KIUME

UKURASA 2


**MICHEZO** NI KARIA, NYAMLANI TENA TFF UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Mhandisi matatani kisa ujenzi wa vyoo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga. Dk. Philemoni Sengati, amemtaka Kaimu Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, William Lisiu, kuandika barua kujieleza kutokana na kushindwa kusimamia vizuri mradi wa ujenzi wa matundu ya vyoo kwenye zahanati na Shule ya Sekondari Solwa wilayani humo.

Sengati alitoa agizo hilo juzi alipozuru kikazi wilayani Shinyanga kwa ajili ya kukagua miundombinu ya sekta za elimu na afya, akiambatana na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa.

Alisema haiwezekani kwenye ujenzi wa matundu ya choo katika shule hiyo ya Solwa na zahanati kuwapo na dosari wakati serikali ilitoa michoro ya ujenzi wake.

Alibainisha kuwa vyoo vimejengwa tofauti na maelekezo na kumtaka kaimu mhandisi huyo ajieleze kwa maandishi.

"Ninaagiza mbomoe vyoo hivi na kuvijenga upya kwa kufuata maelekezo ya serikali, na msiniambie pesa mtatoa wapi," aliagiza.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, aliwataka watumishi wa serikali kuwa waaminifu kwenye usimamizi wa miradi ya serikali, ili itoe huduma bora kwa wananchi.

Kaimu Mhandisi Lisui aliahidi kutekeleza maagizo ya mkuu wa mkoa na kufanyia marekebisho ya ujenzi wa matundu hayo ya choo kwa kufuata michoro iliyotolewa na serikali.

# Ukweli kuhusu chanjo corona nguvu za kiume

**Na Mary Geofrey**

WATAALAMU wa afya nchini wamebainisha hakuna uhusiano kati ya chanjo na kuongeza nguvu za kiume.

Mkurugenzi wa Kuratibu Utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dk. Paul Kazyoba, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu chanjo ya UVIKO-19.

Alisema hakuna utafiti uliofanywa kuhusu uhusiano wa chanjo ya Johnson & Johnson inayotolewa nchini na kuongeza au kupunguza nguvu za kiume.

"Licha ya kuwa hakuna utafiti uliofanywa kwetu sisi wanaume tuliochanja, mimi binafsi sikuona mabadiliko yoyote kuhusu nguvu za kiume kama ni hasi au chanya, kwa maana hiyo ninaweza kusema chanjo hii haina uhusiano na suala hili," alisema Dk. Kazyoba.

POMBE MARUFUKU

Kuhusu unywaji wa pombe, Dk. Kazyoba, alisema inashauriwa kuwa anayetaka kuchanja, anapaswa kutokunywa pombe siku tatu kabla na baada ya kuchanja.

"Ni ngumu 'kum-control' (kumdhibiti) mtu mmoja mmoja asinywe pombe lakini ni muhimu wakazingatia hili hasa ikizingatiwa kuwa chanjo haifanyi kazi kwenye mwili wa binadamu mara tu baada ya kuchanja," alisema.

Dk. Kazyoba alisema mgonjwa anayekiuka masharti na kunywa pombe kabla na baada ya kuchomwa chanjo, yupo katika hatari ya kupata madhara kwenye ini.

Alisema kuwa madhara yatajitokeza kwenye ini kwa sababu lina kazi ya kuchuja sumu katika mwili, hivyo litalazimika kuanza kupambana na sumu ya pombe wakati huo huo kupokea chanjo inayoingia mwilini.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mbobezi wa Moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Tatizo Sanga, alisema chanjo huanza kufanya kazi kwenye mwili wa mtu kuanzia siku saba hadi 15.

Alisema baada ya mtu kuchoma chanjo, mwili huanza kujipanga kutengeneza utaratibu wa kuipokea kabla ya kuanza kufanya kazi ndani ya wiki mbili.

**MAGONJWA SUGU**

Kuhusu watu wenye magonjwa sugu kupata chanjo, Dk. Sanga alisema ni muhimu kundi hilo kupewa chanjo ili kuwaepusha na mashambulizi ya UVIKO-19 yanayoweza kuwaweka katika hatari tofauti na wasio na magonjwa hayo.

"Watu wenye matatizo ya moyo ni muhimu kupata chanjo ili waepuke changamoto ya upumuaji inayoongeza shambulizi kwenye mwili na kuleta uwezekano wa mgonjwa kupoteza maisha," alifafanua Dk. Sanga.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mbobezi wa Mapafu na Mahututi, Pauline Chale, alisema wagonjwa wenye maambukizi ya UVIKO-19 hupata madhara kwenye mapafu.

Alisema kuna milango ipo kwenye mapafu, moyo, ini na mfumo wa tumbo ambayo UVIKO-19 huitumia kujishikiza hadi kufika kwenye seli za damu.

Alisema kutokana na mwingiliano huo wa kirusi, mgonjwa hupanwa mapafu na kushindwa kuvuta hewa na ndio sababu ya kumwekea hewa ya Oksijeni ambayo hutumia hadi wiki nne ili kurejea katika hali ya kawaida.

"Kutokana na kuwa mgonjwa anakaa kwenye Oksijeni kwa wiki mbili hadi nne kama hatapoteza maisha, hutumia mitungi mitatu hadi mitano kwa siku, wakati gharama ya kumlaza mgonjwa mmoja kwa siku ni Sh. 500,000, hivyo utaona gharama zilivyo kubwa," alisema.

Dk. Pauline aliwataka wananchi kuendelea kujikinga na kupata chanjo kwa manufaa yao binafsi na vizazi vyao.



Abiria wakiwa wamesongamana wakati wakisubiri kuingia kwenye daladala katika kituo cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, bila kuchukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya ugonjwa wa Corona kwa kuvaa barakoa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC afunguka kiini cha ongezeko vifo Kilimanjaro

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UONGOZI wa Mkoa wa Kilimanjaro umetoa ufafanuzi kuhusu ongezeko la vifo vya watu mkoani humo, ukibainisha kuwa sio wote wanaofariki dunia na kuzikwa, ni wagonjwa wa UVIKO-19, bali maradhi mengine ikiwamo kansa na umri mkubwa.

Vilevile, umeitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) kuwadhibiti watumiaji wa mitandao ya kijamii wanaopotosha taarifa za chanjo ya corona.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, aliyasema hayo jana wakati wa utoaji wa huduma ya chanjo ya corona iliyoanza Agosti 3 na hadi jana, mkoa huo ukipokea dozi 60,000.

Alibainisha kuwa hadi jana, tayari wananchi 10,300 walikuwa wamepatiwa chanjo katika mpango huo wa awali uliolenga wataalamu wa afya, watu wenye maradhi sugu na wenye umri wa kuanzia miaka 50.

"Takwimu zinaonyesha kuwapo kwa wagonjwa hao (wa UVIKO-19), lakini haina maana kila anayeumwa lazima afe, Ikumbukwe wakazi wa Kilimanjaro ni watafutaji, wametapakaa nchi nzima na wanapofariki dunia huletwa mkoani hapa kwa ajili ya maziko kwa mujibu wa utamaduni wao," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Kilimanjaro (CCM), Patrick Boisafi, aliwataka wanaKilimanjaro kujitafakari upya kuhusu uzikaji hasa kwa walioko nje ya mkoa huo.

"Wajitafakari upya kama kuna uwezekano wazike huko huko na wakisafirishwa, basi waje wachache.

"Kuna lugha inayotembea kwenye mitandao kuwa Mkoa wa Kilimanjaro ndio unaoongoza kwa watu wengi kufa, lakini tukumbuke utamaduni wao.

"Gharama ya kutibu ugonjwa huu ni kubwa kuliko kuchanja, hivyo ni vyema kila mmoja wetu ajitokeze katika kupata chanjo ili kukabiliana na ugonjwa huu, tuachane na upotoshaji wa kwenye mitandao," alisema.

Baadhi ya waandishi wa habari waliojitokeza kuchanja, akiwamo Nakajumo James, walisema kutokana na kazi wanazofanya, inawalazimu kupata chanjo hiyo.

"Ni lazima serikali iangalie namna ya kuhamasisha na kutoa elimu sahihi juu ya chanjo ili kuondoa upotoshaji kuanzia ngazi ya vitongoji," alisema Martha Fatael, mwandishi wa habari.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kagaigai, na mkewe ni miongoni mwa walioongoza kupata chanjo mkoani hapa.

Viongozi wengine waliojitokeza ni Mwenyekiti wa CCM mkoani hapa, Boisafi na mkewe, Katibu Tawala wa Mkoa, Dk. Seif Shekalaghe, na viongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wakuu wa wilaya, wakuu wa taasisi zilizopo mkoani hapa.

Jana, Nipashe iliripoti kuhusu kuadimika kwa majeneza mkoani Kilimanjaro kulikotajwa kusababishwa na ongezelo la uhitaji wa huduma za mazishi mkoani humo.

## HABARI KITAIFA

# Wastaafu wafundwa matumizi mafao yao

**Na Christina Mwakangale**

WASTAAFU watarajiwa wametakiwa kuzitumia fedha zao za mafao kwa kuwekeza katika miradi, viwanda vidogo na kutoa ajira kwa vijana ili kukabili uhaba wa ajira uliopo nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alitoa wito huo juzi alipofunga semina kwa wastaafu watarajiwa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) jijini Dar es Salaam.

Alisema wastaafu watarajiwa hao kupitia semina hizo ambazo zilishirikisha taasisi mbalimbali katika kuwapa mafunzo, ziwe chachu kwao na kutumia vyema elimu waliyoipata kutunza fedha baada ya kupata mafao yao.

Mhagama aliwataka PSSSF kuwa na mafunzo endelevu kama hayo kwa kuwa wanachama walio wengi hawana elimu ya kutosha ya usimamizi wa fedha na ubunifu wa miradi ili kujipatia kipato baada ya kustaafu.

"Kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo wastaafu wamekuwa wakikutana nazo baada ya kustaafu, kati ya hizo kubwa ni namna bora na sahihi ya kutumia fedha wanazolipwa baada ya kustaafu.

"Mfuko wa PSSSF kwa kushirikiana na wadau waliamua kuja na mpango wa kutoa mafunzo kwa wastaafu watarajiwa ili waweze kupata uelewa juu ya matumizi sahihi ya fedha hususan katika usimamizi wa uwekezaji wao binafsi wanaofanya wastaafu wetu," alisema Mhagama.

Waziri huyo alisema mifuko iwaelekeze wastaafu na wanachama namna ya kupata huduma bora ikiwa ni pamoja na elimu ili kuepukana na matapeli na upotevu wa fedha wanazowalipa.

"Kumeibuka wimbi la matapeli wanaowasiliana na wastaafu kwa njia ya simu, wanawapigia simu wazee kuwataja majina yao na kutaja taarifa zote za mstaafu.

"Madai ya matapeli hao ni kwamba wao ni watumishi ama wa mfuko wa pensheni ama benki na wanadai wanashughulikia mafao ya mstaafu wanayempigia.

"Kwa bahati mbaya baadhi ya wastaafu wetu wamekuwa wakituma fedha hizo na kuishia kutapeliwa.

"Ninaomba menejimenti za mifuko na wakuu wa benki zetu leo tujiulize, matapeli hawa wanapatiwa taarifa na nani? Niwaagize wote kuwa makini na suala hili," alionya.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, katika hotuba yake, alisema mifuko ya pensheni hulipa wastaafu fedha nyingi kwa mkupuo, ambazo mstaafu akizitumia vizuri, zitaleta tija katika maisha yake ya ustaafu.

Alisema fedha hizo zitasaidia kuendeleza miradi mbalimbali ya mstaafu, kutoa ajira kwa vijana na kuboresha hali ya maisha na kumwezesha kujikimu yeye pamoja na familia na kuleta manufaa kwa taifa.

Kashimba alisema mfuko huo pamoja na kutoa semina kwa wastaafu kutunza fedha, pia wametoa elimu kuhusu ujasiriamali, kuwekeza miradi ili wajikimu baada ya kustaafu.

Alisema PSSSF imeanzisha mfumo maalum kupitia simu za mkononi ambao mwanachama ataweza kupata taarifa kuhusu michango.

Semina hiyo ilishirikisha taasisi za kifedha zikiwamo TBP, NMB, NBC, CRBD, DCB, Azania, ABC, MCB pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na Mfuko wa UTT AMIS.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekta ya Afya, Dk. Grace Maghembe, akikata utepe kuzindua mradi wa kupunguza maambukizi ya kifua kikuu unaotekelezwa na Shirila la Afya la AMREF kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkazi AMREF Tanzania, Dk. Florence Temu na Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi AMREF, Dk. Eric Van Praag (kulia). **PICHA: MARY GEOFREY**

# RC Arusha waweka zuio kutembeleana kisa corona

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

KANISA Katoliki Jimbo Kuu la Arusha limetangaza kusitisha makongamano yote na kutembeleana kati ya parokia na parokia jimboni humo kuanzia leo kutokana na kile lilichodai mwelekeo wa hali mbaya zaidi ya maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Kwa mujibu wa waraka wa Askofu Mkuu Jimbo hilo, Isaac Amani, ulioandikwa kwa mapadre, watawa na Halmashauri ya Walei na uliosambaa kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii ya vikundi vya kidini jimboni Arusha jana, kuna hadhari kuwa hali ya ugonjwa UVIKO-19 ni mbaya na inaelekea kuwa mbaya zaidi.

Waraka huo uliotiwa saini na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, Amani, unabainisha:

"Jimbo Kuu Katoliki la Arusha tunasitisha kuanzia kesho (leo) tarehe 8 Agosti, 2021, makongamano yote na ziara za kutembeleana kati ya parokia na parokia. Tumwombe Mungu atulinde, sisi wenyewe tusijiingize hatarini."

Nipashe ilimtafuta Askofu Amani na akathibitisha kuwa waraka huo ni wake na utasomwa leo katika parokia zote za Jimbo Kuu Katoliki la Arusha.

Ndani ya wataka huo, Askofu Amani anawataka wamumini na watawa kusoma alama za nyakati, kutodharau wala kupuuzia tahadhari na maelekezo yanayotolewa na viongozi, Wizara ya Afya na serikali.

"Daima tukumbushane: Kinga ni bora kuliko tiba. Tusiyafumbie macho yanayotokea mbele yetu, hali itakaporuhusu tutarudia hali ya kawaida," Askofu Amani anasema katika waraka wake huo.

Anahimiza waumini kuwa makini wanapojumuika kwenye makundi ili kuepusha maambukizi, kila mmoja kulinda nafsi yake kwa kuwa hajulikani nani aliyeambukizwa UVIKO-19 na asiye na maambukizi.

"Anayepinga mamlaka ya wiongozi, anapinga agizo la Mungu, nao wafanyao hivyo, wanajiletea hukumu wenyewe," waraka huo ulinukuu maandiko matakatifu ndani ya Biblia.

Hata hivyo, kwa mujibu wa waraka huo, mikutano ya sala kwa kila parokia au vigango pamoja na sala za jumuiya ndogondogo zitaendelea lakini kwa kuzingatia umbali, usafi na kukutana kwenye eneo la wazi lenye mzunguko mzuri wa hewa safi.

"Ninawatakia wakulima wote baraka na fanaka tele tunapoadhimisha Sikukuu ya Wakulima. Mwenyezi Mungu atujalie mavuno mengi na maisha bora," Askofu Amani anasema katika waraka wake huo.

# AMREF yafadhili vifaa kukabili TB

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la AMREF Tanzania linalojishughulisha na utoaji wa huduma za afya kwa jamiii, kupitia mradi wake wa USAID Afya Shirikishi, limetoa msaada wa baiskeli 710 na vikasha 859 vya kubebea sampuli za kufanyiwa vipimo vya kifua kikuu (TB) katika mikoa tisa nchini.

Mradi huo wa miaka mitano unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) nchini kwa ajili ya Watumishi wa Afya (CHWs) walio katika mikoa ya Dar es Salaam, Geita, Katavi, Kigoma, Mwanza, Pwani, Rukwa, Songwe, Kaskazini Unguja na Mjini Magharibi visiwani Zanzibar kuwafuata wagonjwa nyumbani.

Mkurugenzi Mkazi wa AMREF nchini, Dk. Florence Temu, akizungumza katika hafla ya makabidhiano yaliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam, alisema lengo la mradi huo ni kuwapata wagonjwa wanaougua kifua kikuu, kuwatibu na kuhakikisha wanapona.

Alisema baiskeli hizo zitawawezesha wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kuongeza upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora wa juu zilizo kamilifu na fungamanishi katika jamii zao kwa kuimarisha utoaji wa huduma za afya za kifua kikuu.

"Hii itapunguza muda uliotumika na umbali na kurahisisha ubebaji wa sampuli zinazohitaji kupimwa kwani ubebaji huu utahakikisha kwamba sampuli hizo zinafika katika vituo vya kukusanyia katika muda sahihi na kwa usalama," alisema.

Alifafanua kuwa mradi huo unalenga kupunguza maambukizi na kuendelea kwa TB kupitia uimarishaji wa utoaji huduma katika ngazi ya jamii, kuimarisha upatikanaji na matumizi ya huduma bora za uzazi wa mpango, kuimarisha uwazi, utoaji mrejesho na upatikanaji wa takwimu zinazohusiana na programu za TB.

"Utasaidia sana kuimarisha sera na miongozo ya taifa ya TB na kuongeza uongozi na uungaji mkono wa kisiasa katika vita dhidi ya TB kama kipaumbele cha jamii," Dk. Florence alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo utashughulikia mahitaji ambayo bado hayajatimizwa kuhusu uzazi wa mpango kupitia afua za kijamii katika mikoa minne ya Katavi, Kigoma, Rukwa na Songwe.

Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya ya Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa USAID, Ananthy Thambinayagam, alisema Serikali ya Marekani itaendelea kuisaidia na kushirikiana na Serikali ya Tanzania, washirika wa maendeleo, Asasi za Kiraia (AZAKI) na wadau wengine kufanya kazi pamoja kuimarisha mfumo wa afya nchini.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Grace Maghembe, akizindua mradi huo, aliipongeza AMREF katika kupambana na TB nchini.

"Kupitia Wizara ya Afya, tunashukuru kwa baiskeli hizi na vikasha hivi vya vibebea sampuli za makohozi ya TB ambavyo vitatumika katika mikoa inayotekeleza mradi huu nchini," alisema Dk. Grace.

RIPOTI MAALUM

## UGORO, TUMBAKU

# Janga lingine la kiafya nchini

**•Muhimbili: 80% wanaougua saratani ya mapafu ni waraibu wa tumbaku •Kila wiki kuna wagonjwa wapya saba**

**Na Mary Geofrey**

KUMEIBUKA biashara ya ugoro kwenye maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam inayofanyika sambamba na uuzwaji wa vinywaji vikali katika maeneo husika.

Uchunguzi wa Nipashe Jumapili uliofanyika kwa wiki kadhaa katika mkoa huo wa kibiashara, umebaini biashara hiyo imeshamiri kwenye baadhi ya maeneo yakiwamo Mwenge kwa wauza vinyago, stendi za daladala Segerea, Kinyerezi na Mbezi Mwisho.

Wakati biashara hiyo ikizidi kushika kasi mkoani humo, wataalamu wa afya wamebainisha kuwa matumizi ya ugoro na bidhaa zingine zitokanazo na tumbaku ni hatari kiafya.

Licha ya serikali kulitazama zao la tumbaku kuwa miongoni mwa mazao yanayotegemewa kibiashara na kiuchumi nchini, takriban watu 600,000 hufariki dunia kila mwaka kutokana na kuvuta moshi wa sigara kwa kuwa karibu na wavutaji huku asilimia 28 kati yao wakiwa ni watoto.

Wakati idadi hiyo ya vifo ikiendelea kuwa tishio, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetenga zaidi ya asilimia 40 ya bajeti yake kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza.

Kati ya magonjwa yasiyoambukiza yanayolitesa taifa, asilimia kubwa yanasababishwa na matumizi ya bidhaa zitokanazo na tumbaku.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mfumo wa Upumuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Alex Masao, katika mazungumzo maalum na Nipashe kuhusu magonjwa yasiyoambukiza, anabainisha madhara yanayosababishwa na matumizi ya ugoro na bidhaa zingine zitokanazo na tumbaku.

Anasema mtu anayetumia tumbaku kwa muda mrefu anaingiza sumu mwilini, ambayo huchangia tatizo la upumuaji na saratani ya njia ya upumuaji.

Mtaalamu huyo anasema kwenye tumbaku kuna kemikali inayoitwa 'nicotine' inayosababisha mtu kuathirika kwa kuwa na uraibu na kumfanya aendelee kutumia bila kuacha.

Anasema matumizi ya tumbaku pia yanaweza kusababisha madhara nje ya mfumo wa upumuaji kama moyo na mishipa mikubwa ya fahamu.

Kwa kulinganisha na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania, anasema matumizi ya tumbaku ni asilimia ndogo kulinganisha na nchi zilizoendelea.



Kijana mchuuzi wa ugoro akiandaa bidhaa yake wakati akisubiri wateja katika eneo la Kitunda Kivule, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Anatoa angalizo kuwa licha ya nchi kuwa na asilimia ndogo ya watumiaji wa tumbaku, asilimia 80 ya wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa upumuaji na saratani wanakuwa na historia ya kutumia tumbaku kwa miaka 10 hadi 15 iliyopita.

"Unakuta ametumia tumbaku miaka ya ujanani lakini anakuja hospitali ameshaacha kutumia na anakuwa na tatizo hili," anafafanua Dk. Masao.

Anasema wenye matatizo ya mfumo wa upumuaji huwa ni watu wenye umri kuanzia miaka 55 kwenda juu na ndio ambao wanafika kwa wingi hospitalini huko.

Dk. Masao ambaye anahudumia wagonjwa wa aina hiyo, anasema kwa wiki katika kliniki ya mapafu, wanapokea wastani wa wagonjwa wapya watano hadi saba wenye matatizo ya kutumia tumbaku kwa muda mrefu.

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji kutokana na hostoria ya kutumia tumbaku, hayatibiki moja kwa moja isipokuwa wanapewa dawa za kuwasaidia kupumua.

"Tatizo hili ni sugu, mgonjwa akija hospitalini kwa sababu ni ugonjwa sugu tunampa dawa za kumsaidia kupumua lakini hatuna dawa za kutibu kabisa ugonjwa huu," anasisitiza.

Dk. Masao anabainisha kuwa njia salama ya kuepuka ugonjwa huo ni kutovuta sigara au kutoishi na anayevuta sigara.

Mbali na matumizi ya tumbaku, anasema matumizi ya kuni katika chumba kisicho na mfumo wa kutoa moshi nje ni sababu nyingine ya watu kuugua magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji.

"Kuna wagonjwa wachache ambao wanakuwa wana magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji lakini hawana historia ya kuvuta sigara, ni wachache ambao wana sababu nyingine," anafafanua.

Dk. Masao anataja sababu nyingine ni watu wenye historia kufanya kazi katika viwanda, migodi ya madini, hasa dhahabu na almasi bila kutumia dhana za kujikinga kama maski.

Kuhusu matibabu, Dk. Masao anasema wagonjwa wanafika hospitalini tayari wameshapata madhara kwenye mapafu.

Anasema wagonjwa wanafika hospitalini wakiwa katika hatua ya kati ya tatizo, yaani hawawahi wala hawachelewi sana.

Anabainisha kuwa wagonjwa wanaofika hospitalini wakiwa na matatizo hayo, huanza kuwafanyia vipimo na kubaini mapafu yameshachoka.

Dk. Masao anasema dalili za ugonjwa huo ni kuanza kuchoka unapofanya kazi kidogo, kuishiwa pumzi, kushindwa kutembea kwa muda mrefu na kikohozi kikavu kisichoisha.

Kuhusu takwimu za vifo, Dk. Masao anasema wagonjwa wengi wanafariki dunia kwa magonjwa mengine.

"Kwa sababu magonjwa haya ni sugu, mgonjwa ataendelea na matibabu mfululizo na kinachosababisha vifo ni magonjwa mengine anayopata mgonjwa," anasema.

Dk. Masao anasema kutokana na mapafu kuathirika, nguvu ya kufanya kazi inapungua na kushusha kasi ya uzalishaji kwa wagonjwa na hivyo kuanza kuwa wategemezi.

Kuhusu gharama za matibabu, mtaalamu huyo anasema ni kubwa, lakini kuwapo kwa huduma ya bima kumekuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa.

"Kwa Muhimbili tuna sera yetu matibabu kwanza, fedha baadaye. Kwa hiyo, hatuwezi kusema watu wanakosa huduma kwa sababu ya gharama kubwa za matibabu," anasema.

Anawasihi Watanzania kuepuka matumizi ya tumbaku kama uvutaji wa sigara, kufanya kazi za viwandani kwa kuzingatia tahadhari zote na kuchukua tahadhari katika maeneo hatarishi kama ya migodi.

"Tunasema kinga ni bora kuliko tiba, hivyo ni muhimu Watanzania wakazingatia hili, wagonjwa wakishaumwa ni tatizo sugu lisiloisha mwilini, hivyo ni muhimu wakatambua hili na kuchukua hatua," anaonya.

### UDHIBITI TMDA

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imemepewa jukumu la kudhibiti matumizi ya tumbaku kama uvutaji sigara, ugoro na shisha nchini kuanzia Aprili 30 mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, anasema kwenye tumbaku kuna kemikali 93 hatarishi kwa afya ya binadamu.

Anasema TMDA ina jukumu la kuangalia kiwango cha kemikali hizo kiwe chini ili mtumiaji asiendelee kupata madhara zaidi kwa kutumia tumbaku.

Anasema wameanza kuweka mfumo wa namna ambavyo watadhibiti, kufanya usajili, ukaguzi na upimaji katika maabara zao kama tumbaku zina ubora usioleta madhara kwa watumiaji.

"Kuna mashine ambazo tunaweza kuanza kutumia kuchunguza hizi tumbaku kulingana na nyingine.

"Tutachunguza tukishakuwa na mashine za kisasa zaidi ili kupata kile tunachotaka hasa kujua kiwango cha kemikali," anasema.

Fimbo anaongeza kuwa inafahamika kuwa matumizi ya tumbaku yanasababisha magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu, saratani na mfumo wa upumuaji. Anasema wanatoa elimu ili walioanza kuvuta tumbaku wapunguze kama siyo kuacha kabisa, ambao hawajaanza wasitumie na vijana walio na umri chini ya miaka 18 kutoanza kutumia bidhaa hiyo.

Anabainisha kuwa Sheria ya Kudhibiti Tumbaku inataka pia maeneo yenye mikusanyiko yatengewe maeneo ya kuvutia sigara, yawe na vizuizi ili moshi wa sigara usiwafikie watu wengine.

Anasema pia watafikia wauzaji, waingizaji na watengezaji ili kusaidia kupunguza madhara kwa jamii.

### WANAWAKE HATARINI

Matumizi ya tumbaku nchini yanatajwa kuongezeka miongoni mwa wanawake kulinganishwa na wanaume, hatua ambayo inatajwa kuathiri kwa kiwango kikubwa afya za watoto hasa walio chini ya umri wa miaka mitano.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na serikali, kiwango cha wanaotumia bidhaa za tumbaku kimeongezeka kutoka asilimia 2.9 mwaka 2012 hadi asilimia 3.2 mwaka 2018.

Utafiti huo unabainisha kuwa kundi hilo linalotegemewa katika malezi ya watoto kwenye jamii, watoto wanakuwa kwenye hatari kubwa kutokana kuvuta moshi wa bidhaa za tumbaku kutoka kwa mtumiaji.

Kwa mujibu wa utafiti huo, vijana waliowahi kutumia tumbaku ya aina yoyote ile kwa kipindi cha mwaka mmoja, wanawakilisha asilimia 9.7, hatua inayoifanya Wizara ya Afya kuona inalo jukumu la kuhamasisha kuacha kwa hiyari matumizi ya tumbaku.

### TAKWIMU ZA SERIKALI

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, akiwa katika maadhimisho ya Siku ya Kutotumia Tumbaku Duniani Mei 31 mwaka huu, alibainisha kuwa wastani wa asilimia 14 ya Watanzania wanatumia tumbaku wakati asilimia 2.9 wakiwa ni wanawake kwa mujibu wa takwimu za WHO za mwaka 2018.

Alisema taarifa ya tathmini ya viashiria hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza ya mwaka 2012 ya Wizara ya Afya ilionyesha watumiaji wamepungua kufikia asilimia 8.7 na asilimia 3.2 ya watumiaji ni wanawake.

Waziri huyo alisema utafiti mpya unaonyesha asilimia 8.7 ya watu wazima, sawa na watu milioni 2.6 nchini, wanavuta tumbaku na bidhaa zake.

Alisema utafiti huo pia ulionyesha asilimia 32.9 ya watu wazima walionekana kuvuta moshi wa watumiaji (secondhand smokers) wakiwa wanafanya shughuli kwenye maeneo ya ndani ambao walikuwa sawa na watu wazima milioni moja.

Dk. Gwajima alisema asilimia 13.8 ya watu wazima, sawa na milioni 4.1 wakiwa maeneo ya majumbani, asilimia 31.1 ya watu wazima sawa na watu milioni 3.5 wakiwa kwenye maeneo ya migahawa na asilimia 77 sawa na watu wazima milioni tatu wakiwa maeneo ya baa na kumbi za starehe za usiku.

Alibainisha taarifa nyingine ya uchunguzi wa hali ya matumizi ya tumbaku kwa vijana wa mwaka 2008 uliofanyika nchini, iliyobaini uwiano wa vijana waliowahi kutumia tumbaku ya aina yoyote ile katika kipindi cha mwaka mmoja (2007) ilikuwa asilimia 9.7.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi watano wafa ajali ya bodaboda

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WANAFUNZI watano wa Shule ya Sekondari ya Kimange, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, wamefariki dunia baada ya ajali iliyohusisha pikipiki na gari aina ya Mitsubishi Fuso.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo ambayo alisema ilitokea juzi saa 1: 15 usiku wakati wanafunzi hao wakitoka michezoni wakiwa wamepakizana kwenye pikipiki moja.

Kamanda Wankyo alisema gari aina Mitusubish Fuso lenye namba za usajili T 198 CWN likitokea Dar es salaam kwenda Arusha likiendeshwa na Rasul Meena (33) lilimgonga mwendesha pikipiki na kusababisha vifo vya wanafunzi wanne hapo hapo.

Alisema mwanafunzi mwingine alikutwa na umauti wakati akipatiwa matibabu Hospital ya Jeshi Kihangaiko.

Wankyo alisema wanafunzi hao wa Shule Sekondari ya Kimange walikuwa wamepakiana kwenye pikipiki moja wakitokea Kimange kwenda Mbwewe ambako walikuwa wakishiriki michezo na shule jirani ya sekondari ya Kwamakocho. Aliwataja wanafunzi hao waliofariki dunia kuwa ni Laya Masudi (16) wa kidato cha tatu, Furaha Athumani (16) kidato cha tatu, Athumani Bushiri (15) kidato cha Kwanza, Amina Msomba (15) kidato cha kwanza na Athumani Mchafu (17) Kidato cha tatu.

Kamanda Wankyo alisema chanzo cha ajali hiyo kuwa ni uzembe wa dereva wa gari aliyekuwa akiendesha kwa mwendokasi uliosababisha kushindwa kumudu gari hilo na kusababisha kumgonga mwendesha pikipiki akiyekuwa mbele yake.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, jana alishiriki mazishi ya watoto hao na kutoa pole kwa familia na wananchi wa kata hiyo kwa msiba mkubwa ambao wameupata.

"Kwa niaba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, nitoe pole kwa familia kwa msiba huu mkubwa. Niwaombe tuzingatie matumizi ya vyombo vya moto.

"Kwa upande wa serikali tunaendelea kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria za, nchi na dereva wa gari hilo tunaye tutachukua hatua dhidi yake kwa mujibu wa sheria," alisema Kunenge.

## Mameneja mahiri TPC sasa kuwekwa mikoa ya kimkakati

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Matthew, ameagiza Shirika la Posta Tanzania (TPC) kuhakikisha katika mikoa ya kimkakati na majiji wanawekwa mameneja wenye uwezo mkubwa wa kuchanganua maono ya kidijitali ya shirika.

Mhandisi Matthew aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga kikao cha siku tano cha shirika hilo kilichohusisha mameneja wakuu, wakuu wa idara na vitengo makao makuu, mameneja wa mikoa na viongozi wa vyama vya wafanyakazi.

Alisema kwa sababu shirika kwa sasa ni la kidijitali, ni lazima watendaji wake nao waendane na teknolojia ili kufikia malengo yaliyowekwa.

"Tunasema Posta kiganjani, lazima watendaji nao waende kidijitali wapewe vitendea kazi. Mnatakiwa mwende na mabadiliko. Mapinduzi yanaanzia katika fikra zetu, mafunzo mliyopata mkayafanyie kazi bila kumwonea mtu.

Kaimu Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo, alisema kikao hicho kimefanyika kutokana na wizara kutaka watendaji watie saini mikataba mipya ya utekelezaji wa kazi katika maeneo yao.

"Wamejaza fomu za upekuzi na ufuatiliaji, tumeangalia mikoa iliyofanya vizuri na iliyofanya vibaya na tumempata mfanyakazi bora na tumejadili mwelekeo wa shirika," alisema.




Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikata utepe kuzindua nyumba 50 zilizojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), katika eneo la Buhare, Musoma, mkoani Mara juzi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# NHC yaanza mikakati uwekezaji majengo ya biashara pembezoni

**Na Munir Shemweta,** MUSOMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limeanza mikakati ya kuwekeza majengo ya kibiashara katika maeneo ya pembezoni mwa nchi. Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa nyumba za makazi katika eneo la Buhare, Musoma mkoani Mara uliofanywa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, kama ulivyoelekeza kwamba shirika liwekeze majengo ya biashara maeneo ya pembezoni mwa nchi, tulishaanza kufanya hivyo eneo la Mutukula, Kagera na sasa tunaangalia uwezekano wa kuweka kwenye mpaka wa Kenya na Tanzania," alisema Dk. Banyani.

Kwa mujibu wa Dk. Banyani, NHC inafanya upembuzi yakinifu eneo la Sirari mpakani mwa Tanzania na Kenya na uamuzi huo unatokana na timu iliyofanya ziara katika eneo hilo kukuta upande wa Kenya umechangamka kibiashara kulinganisha na ule wa Tanzania.

Alisema NHC ikiwezeshwa ikiwamo kupatiwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji majengo litafanya mabadiliko makubwa na kutolea mfano wa jengo la TRA lililoko mpaka wa Tanzania na Kenya haliko vizuri kulinganisha na lile la Kenya.

"Ili eneo la Sirari lichangamke kibiashara kama ilivyo upande wa pili, lazima tuwekeze katika majengo ya kibiashara. Lengo hapa kupendezesha mandhari ya mipaka yetu na kukuza biashara kimataifa," alisema Dk. Banyani.

Naibu Waziri Mabula akizungumza katika uzinduzi huo, alisema mbali na mikakati ya shirika kuwekeza majengo ya kibiashara, halmashauri zilizoko maeneo ya pembezoni zinapaswa kuitumia NHC kwa kuipatia ardhi kufanya uwekezaji.

"Pamoja na mikakati ya uwekezaji maeneo ya pembezoni, iko haja ya kulitumia shirika kwa kuliwekea miundombinu mizuri ya kibiashara ili kuwekeza maeneo ya mipakani ambako Tanzania inaonekana iko nyuma ukilinganisha na nchi jirani," alisema Dk. Mabula.

Aidha, Naibu Waziri alielekeza kujengwa shule ya msingi ya serikali katika eneo la Buhare zilipozinduliwa nyumba 50 baada ya kuombwa kutokana na eneo hilo kutokuwa na shule. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari 135 na zilizotumika ni ekari 10 pekee. Dk. Mabula pia alitaka maeneo ambayo NHC inafanya miradi yake, halmashauri husika zihakikishe zinawezesha upatikanaji miundombinu kama vile umeme, maji na barabara kwa lengo la kupunguza gharama za upangishaji au uuzaji wa nyumba za shirika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaopotosha umma kuhusu chanjo ya corona wapuuzwe

**JANGA l**a corona linazidi kuiandama dunia huku watu wakiendelea kukumbwa na maradhi hayo katika wimbi hili la tatu na wengine kupoteza maisha.

Wakati hali ikiendelea kuwa tete duniani kote, nchi mbalimbali zinachukua hatua madhubuti kupambana na janga hilo ikiwamo kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya kama vile kuepuka misongamano isiyo ya lazima, kukaa umbali wa mita moja au zaidi kati ya mtu na mtu, kutumia vitakasa mikono na kunawa kwa maji tiririka na sabuni.

Sambamba na afua hizo, madhehebu ya dini nayo yametakiwa kuhakikisha watu wanafuata kanuni za afya na wakati huo huo ibada zinakuwa fupi ili kuepusha uwezekano wa kuwapo maambukizi ya corona. Kadhalika katika vyombo vya usafiri imeamuriwa watu wakae kwenye viti na viache kujaza watu licha ya kwamba agizo hilo kwa Dar es salaam linaonekana kama mfupa uliomshinda fisi.

Kubwa zaidi, serikali imezindua chanjo dhidi ya corona na uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwaongoza viongozi wakuu na waandamizi wa serikali pamoja na wale wa siasa na dini kupata chanjo hiyo. Baada ya hapo, chanjo hiyo imesambaa mikoani kote huku wakuu wa mikoa na waandamizi wao wakiwaongoza wananchi kupata huduma hiyo.

Wakati chanjo hiyo ikiendelea na wananchi wakijitokeza kwa wingi katika vituo vilivyotengwa kwa ajili ya huduma hiyo, kumekuwa na matamko mbalimbali yanayotolewa na baadhi ya watu yakiwamo ya kukatisha tamaa.

Baadhi ya watu, wakiwamo viongozi wa dini wamekuwa wakiwataka wananchi wasikubali kuchanjwa huku wakidai kwamba kuna madhara ambayo yanaweza kujitokeza miaka ijayo. Pia ziko propaganda kwamba chanjo hiyo imeletwa kwa ajili ya kupunguza idadi ya watu Afrika, Tanzania ikiwamo.

Hata hivyo, pongezi nyingi wanastahili viongozi wa serikali wakiongozwa na Rais Samia ambao wameweka bayana kwamba matamshi hayo ni ya uongo na yanalenga kuwapotosha watu ili wasipate huduma hiyo na matokeo yake waangamie.

Pamoja na kuwapo kwa jitihada za kuwataka Watanzania kuwapuuza watu hao, kumekuwapo na maneno ya kutia chumvi kwamba chanjo hiyo inafaida hasa katika kuimarisha nguvu ya mwili. Kiongozi mmoja wa dini aliibuka na kusema baada ya kuchanja, 'mambo yake ya ndani' yameimarika! Lakini wataalamu wa afya wameweka wazi kwamba hakuna uhusiano wowote kati ya chanjo na tendo la ndoa.

Kubwa na la msingi, ni kwamba Watanzania katu wasiyumbishwe na maneno ambayo yana mwelekeo wa upotoshaji na kukwamisha mpango mzima wa serikali kuhakikisha kila mtu anapata chanjo dhidi ya corona.


Watanzania wanapaswa kutambua kuwa ugonjwa huo unafyeka mamilioni ya watu kwa kasi, hivyo kama hatua madhubuti hazitachukuliwa, ni dhahiri wengi wataangamia kwa kudanganywa au kutokuchukua tahadhari kama wataalam wa afya wanavyosisitiza.

Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, aliwahi kusema akili za kuambiwa changanya na zako. Kwa mantiki hiyo, si kila mtu anachosema ni sahihi, hivyo anayepewa taarifa anapaswa kuitafakari na kufanya uchambuzi wa kina kama ina ukweli ndani yake. Baada ya kujiridhisha kuwa ni sahihi mhusika anapaswa kutekeleza na kama haina ukweli aipuuze.

Kwa mantiki hiyo, si kila kitu mtu anachoambiwa kina ukweli. Ndivyo ilivyo kwa suala la chanjo ya corona ambapo Watanzania wanapaswa kuwapuuza wale wanaodanganya kwamba chanjo hiyo ina madhara. Kila mtu afunguke na kutafuta ukweli badala ya kudanganywa.

Kama alivyosema Rais Samia na viongozi wengine wanavyosisitiza, kila mtu achukue hatua na kupata chanjo ya corona ili kujikinga na kusalimisha maisha yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamii inatakiwa kutii mwongozo kudhibiti corona kwa shuruti?

Na Sabato Kasika

**TANGU** kuibuka kwa wimbi la tatu la ugonjwa wa corona, serikali imeshatoa miongozo mbalimbali kwa lengo la kuwanusuru Watanzania dhidi ya ugonjwa huo unaoendelea kuteketeza maisha ya watu duniani.

Miongoni mwa miongozo hiyo ni ule mpya uliotolewa hivi karibuni na wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania, ukielekeza njia kadhaa za kujikinga na ugonjwa, ikiwamo kupiga marufuku mabasi kujaza abiria.

Mwongozo huo unaelekeza vyombo vya usafiri kama mabasi yakiwamo ya daladala, kubeba abiria kulingana na idadi ya viti (level seat) na pia kuwataka abiria kuvaa barakoa na kunawa maji tiririka.

Hata hivyo, pamoja na kuwapo mwongozo huo, watu wengi wakiwamo abiria, makondakta na madereva wa daladala, hasa wa jijini la Dar es Salaam, ni kama wameamua kutouzingatia.

Kwa wakazi wa Dar es Salaam, watakubaliana na hiki kwamba, bado daladala zinajaza abiria kupitia kiasi kama kawaida, wengi wakiwa hawajavaa barakoa, hali ambayo inaweza kuendelea kuchangia maambukizi ya ugonjwa huo hatari.

Ninaamini kwamba, wengi wao watakuwa wamesoma au kusikia kilichomo kwenye mwongozo huo, lakini ajabu wapo wasiochukua hatua au kuzingatia maelekezo yaliyomo, badala yake wanaendelea kuhatarisha maisha yao.

Mbali na mwongozo huo, hata Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam nayo imeingilia kati na kuwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwaelekeza madereva na makondakta kuuzingatia.

Hatua za kamati hiyo zinatokana na ulegevu wa usimamizi katika baadhi ya maeneo, ambapo polisi, wakuu wa wilaya na Mamlaka ya Uthibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), wanatakiwa kusimamia ipasavyo mwongozo wa serikali.

Kamati hiyo inataka kuepuka ubebaji abiria wasiovaa barakoa na hata kuwajaza kupita kiasi, lakini pia kwa wanafunzi, kila daladala iwe inachukua watano watakaosimama, na wawe wamevaa barakoa.

Katika kikao hicho kilichoketi mwanzoni mwa wiki hii, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, anawataka watu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, na ikitokea ulazima, taratibu zote za kujikinga na corona zizingatiwe.

Maelekezo ya mwongozo na ya mkuu huyo wa mkoa ni kama bado hayajazaa matunda na inawezekana kuna haja ya kuchukua hatua zaidi ili kunusuru afya za wahusika dhidi ya ugonjwa huo.

Kinachoendelea ndani ya baadhi ya daladala, kinaashiria kuchukuliwa kwa hatua zaidi ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaweza kusaidia Watanzania kubadilika na kuchukua hatua.

Miongoni mwa hatua ambazo ninadhani zinaweza kuwa ni kuhakikisha watu wanatii sheria kwa shuruti, hasa baada ya kuonekana wazi kwamba wamekuwa wagumu kutii bila shuruti.

Baadhi ya watu hutafsiri neno utii kama kitendo cha kukubali kufanya maelekezo au maagizo ambayo mtu hupewa na aliye na mamlaka ya juu zaidi yake bila kujali kama anakubaliana nayo au la. Neno hilo katika kamusi ya Kiswahili sanifu, limetafsiriwa kwa kifupi tu kwamba, ni nidhamu au adabu ya tabia. Hivyo inapotokea mtu hatii kile anachoelekezewa na mamlaka za juu yake, huyo anataka kushurutishwa.

Inaweza kuwa hivyo kwani asiyetii atakuwa hana nidhamu au utii wa tabia na pia hakubali maelekezo na maagizo anayopewa na aliye na mamlaka ya juu zaidi kuliko yeye, jambo ambalo ni kosa.

Wale wote ambao hawajatii maelekezo, maagizo, kulingana na jinsi wanavyotakiwa kufanya, maana yake ni kwamba, wanataka kushurutishwa ili watii kwa lazima badala ya kufanya kwa hiari.

Takwimu za ugonjwa huo zimeshawekwa wazi na waziri anayeongoza wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania, Dk. Dorothy Gwajima, kwamba idadi ya waliombukizwa corona na kujulikana rasmi wamefikia 682.

Kumekuwapo na miongozo ya kudhibiti ugonjwa huo nchini, ambao kila Mtanzania anatakiwa kuifuata, lakini kinachoendelea kwenye baadhi ya maeneo. ni kama watu wanataka washurutishwe ndipo waifuate.

Ingekuwa jambo jema iwapo kila mmoja wetu kama ataacha mtindo wa kutaka kushurutishwa, badala yake ajifunze kutii maelekezo, maagizo, taratibu, kanuni na sheria bila kusubiri mamlaka husika kutumia nguvu.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kiongozi anayepinga chanjo ni msaliti



Na Pascal Mayalla

**Je, viongozi wetu wote wa umma, wanajua kuwa baada ya nchi kuikubali chanjo na Rais Samia na viongozi wakuu kuchanja, kiongozi yeyote wa umma, anayeipinga chanjo hadharani, kitendo hicho ni Insubordination?**

KWA vile utoaji chanjo ya Uviko unaendelea, kwa Maslahi ya Taifa naendelea kujikita kwenye chanjo, leo nikiangazia hoja ya uhiari wa Chanjo. Japo chanjo ni hiari, hiari ya chanjo ni hiari ya consent (makubaliano) kama ilivyo kwenye mahusiano ya ndoa, ndoa ni hiari, na sio ule uhiari wa choice (kuchagua) kama kwenye uchaguzi, mtu uko huru kujiandikisha kupiga kura, au kutokujiandikisha, na hata ukijiandikisha, bado uko huru kupiga kura au kutokupiga kura, hiyo na uhiari wa choice, lakini uhiari wa chanjo ni uhiari wa consent, kama ulivyo uhiari wa kuingia kwenye mahusiano ya ndoa, ukiisha ridhia kuingia kwenye ndoa, uhiari wa ndoa unaishi hapo, kinachofuata ni wajibu, kuihudumia ndoa sasa inakuwa sio hiari tena, ni wajibu, mwanamume lazima awajibike kumhudumia mkewe, sio hiari ni wajibu, na wanandoa hao wana wajibu wa kuihudumia ndoa, ndio maana kwenye ndoa za kiafrika kuna baadhi ya malalamiko ya wanawake wa kizungu, huku kwetu huwezi kuyasikia.

Wenzetu wazungu, hata baada ya kuingia kwenye ndoa, ili mwanandoa kupata huduma za kindoa, lazima aombe tena ruhusa, aridhiwe ndipo akubaliwe, hivyo hiari inaendelezwa hadi kwenye huduma wakati ni wajibu.

Hivyo ndivyo ulivyo uhiari wa kwenye hii chanjo ya Uviko, kwa vile lengo la chanjo ni kinga, kuzuia kuenea kwa Uviko, una chanja ili kujikinga wewe na kuwakinga wengine, mtu unapokataa kuchanja, sio tu unahatarisha maisha yako, bali una hatarisha kuwaambukiza wengine, hii ya kuwakinga wengine sasa sio choice, ni wajibu. Ili kupata chanjo ile hiari ni kwenye kuridhia tu, yaani ku consent, na sio hiari ya choice kuamua uchanjwe au usichanje, hivyo baada ya nchi kukubali chanjo, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Amiri Jeshi Mkuu, wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe Rais Samia Suluhu Hassan Kuchanja, akifuatiwa na viongozi, kitendo hicho japo ni hiari, hiyo ni silent marching order, amri ya kimya kimya, hivyo viongozi wote wa umma, wana wajibu wa kuchanja, sio hiari! Je, viongozi wetu wote wa umma, wanajua, kuwa baada ya nchi kuikubali chanjo na Rais Samia na viongozi wakuu kuchanja, kiongozi yeyote wa umma, anayeipinga chanjo hadharani, kitendo hicho ni Insubordination?

**True story yangu na insubordination.**

Mimi nilikuwa mtumishi wa umma pale TBC, enzi hizo TVT, nikiendesha vipindi vya siasa, "Ulingo wa Siasa", tayari nchi yetu ilikuwa ndani ya mfumo wa vyama vingi, hivyo mtu kuwa mtumishi wa umma, hakuna ulazima kuulizwa uko chama gani.

Wakati Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, katika vipindi vyangu niliwakaribisha wanasiasa. Kwa vile CCM ndio chama tawala na Tanzania tunaingia chaguzi zote huku CCM ikiwa tayari na uhakika wa ushindi, hivyo nikiwaalika wagombea wa CCM kwenye urais, wanakuwa busy, after all si uhakika wa ushindi upo, ila ukiwaita wapinzani ni fasta.

Baadhi ya watu wakajenga dhana kuwa huyu mwendeshaji wa kipindi, Pasco Mayalla ni pro-oppostion, anawapendelea wapinzani! Hawajui kuwa ukiwaalika CCM, wanakuwa busy. Nikaenda kupiga kambi Zanzibar, huko nako hali ni ile ile kwenye wagombea urais.

Kiongozi wa Umma kupinga chanjo hadharani sio tu ni usaliti, bali pia ni insubordination!

Kwenye vita yoyote ya kitaifa, kama ilivyo vita ya corona, ili kushinda vita, viongozi wote, lazima wasimame pamoja na kuwa kitu kimoja na kuzungumza kwa kauli moja (must stand as one

Tanzania kama taifa likiisha kubali chanjo ya Covid ndio maslahi ya taifa, viongozi wote wa umma, wanakuwa bind na a collective responsibility clause, they must support, msimamo wa serikali.

Na kama kuna kiongozi yeyote wa umma, hukubaliani na chanjo, hakubaliani na msimamo huo wa serikali, wa kuhimiza Watanzania tuchanje, kiongozi huyu unapaswa kunyamaza kimya.

Kama rais amesema tuchanje, anahimiza Watanzania tujitokeze kwa wingi kwenda kuchanja, sio tu ili kujikinga sisi wenyewe, bali kuwakinga wengine na kulikinga taifa, kitendo cha kiongozi yeyote wa umma, kujitokeza hadharani, kuwapotosha Watanzania tusichanje, huku ni kwenda kinyume cha rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni highest order of insubordination ambayo haipaswi kuvumiliwa au kufumbiwa macho.

Kitendo cha kupingana na msimamo wa serikali wazi wazi ni usaliti.

**Wasalaam
Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kelele za Katiba Mpya mpaka lini?



Na Joseph Kulangwa

**Uchaguzi Mkuu ulipofika mwaka jana, wahanikiza Katiba Mpya waliona kilichojiri, hawakuambulia kitu. Kumbe jamaa walinyamazishwa ili kujipanga na kuzoa kila kitu mpaka wakaona aibu na hivyo kuchonga wale wa Uviko-19 ili ionekane na wahanikizi nao wamo bungeni.**

KUNA kelele zinasikika, si kila mahali, bali huku na kule. Kelele za Katiba Mpya. Wanaohanikiza wanasema muda wa Katiba Mpya ni sasa. Wanaosikiliza wanasema muda si sasa, tunaomba muda!

Basi ni kelele kwa kwenda mbele na wanaohanikiza ni wale ambao miaka mitano iliyopita, walikuwa na zipu midomoni walizoshonewa na JPM, aliyesema sitaki kusikia wala kuona, nataka kutekeleza miradi, hivyo subirini uchaguzi mkuu.

Uchaguzi Mkuu ulipofika mwaka jana, wahanikiza Katiba Mpya waliona kilichojiri, hawakuambulia kitu. Kumbe jamaa walinyamazishwa ili kujipanga na kuzoa kila kitu mpaka wakaona aibu na hivyo kuchonga wale wa Uviko-19 ili ionekane na wahanikizi nao wamo bungeni.

Sasa alipoondoka JPM akainigia Samia Suluhu Hassan, wahanikizi wakaona sasa ni muda mwafaka maadam Mama keshasema tusahau yaliyopita tugange yajayo, kwa kuwa yaliyopita si ndwele, basi hapahapa ndipo pa kuibukia na Katiba Mpya.

Wakadhani itakuwa Kitonga tu Mama akiambiwa atakubali, kwa kuwa alikuwa Makamu Mwenyekiti wa lile Bunge maarufu la Katiba, ambalo hatimaye lilikosa umaarufu likaja kuwa maharufu.

Lakini kwa nini watu wanataka Katiba Mpya sasa? Nimetafakuri nikadhani kuwa si kweli kwamba wanahitaji Katiba Mpya kikamilifu, bali hata kukifanyika marekebisho fulani fulani tu watakubali. Kilio kikubwa ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC).

Wanasema ukiwasikiliza vizuri, kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliwafanya mbaya mwaka jana, ndiyo sababu wakakosa kila kitu na kubakiwa na Uviko-19 tu, ambao nao bado dawa yao imo jikoni, kwa mujibu wao.

Hivi kwani ikikubalika tu, kwamba hebu tufanye vijirekebisho vidogo ndani ya Katiba nini kitaharibika? Tuanze basi na INEC, ili Mwenyekiti wake na makamishna wote wasiteuliwe na Rais anayetokana na chama cha siasa, ili wasimpendelee na chama chake!

Hebu tuone, hivi katika hii mihimili mitatu mikuu ya Dola; Serikali, Bunge na Mahakama, kwa nini katika wakuu wao, ni mmoja tu ndiye asiyechaguliwa na wananchi? Kwa nini Jaji Mkuu hatokani na kura za wananchi kama ilivyo kwa Rais na Spika?

Rais anapigiwa kura moja kwa moja na wananchi, tena baada ya kuzunguka nchi nzima akipiga magoti na kuwaomba kura. Spika yeye huchaguliwa na wananchi kupitia wabunge, ambao wamechaguliwa na wananchi, hivyo wanawawakilisha. Jaji Mkuu je?

Hivi kwa nini basi Katiba isirekebishwe na hapo, ili Jaji Mkuu naye achaguliwe na wananchi hata kama si moja kwa moja, ila kwa kupitia chombo chochote kinachowakilisha wananchi? Mathalan itangazwe nafasi, waombe wenye sifa, kisha majina yapelekwe hata bungeni, wabunge wawapigie kura mshindi ndiye awe.

Hivi kwa nini hilo nalo lishindikane, mpaka tuanze kutoleana macho na kukoholeana kipindi kama hiki cha Uviko-19? Juzi kati hapa wenzetu nchi jirani Kenya walifanya hayo kwa Jaji Mkuu wao, watu waliomba kazi na kuchujwa, hatimaye kupigiwa kura na kupatikana Jaji Mkuu.

Haiswihi hata kidogo, kuona wakuu wawili katika mihimili mikuu ndio watokane na wananchi, lakini mmoja tu ateuliwe na mtu mmoja ambaye ndiye mkuu wa nchi, ambaye hatimaye hugombea sambamba na chama chake na pale chama chake kifikishwapo mahakamani hata kama kikishinda kwa haki, hutiliwa shaka.

Hutiliwa shaka, kuwa kimeshinda kesi kwa kuwa mwenyekiti wake ni Rais ambaye humteua Jaji Mkuu, hivyo Mahakama kuwa chini ya Rais na kamwe haiwezi kumwangusha hata iweje, yaani hata chama kikishindwa basi huwa kimeshinda.

Hizo ni hisia tu, ambazo hutoka kwa wananchi wanaotafakari kwa kina na kuona pengine hakuna haki inayotendeka au kuonekana kutendeka, kama uteuzi utaendelea kutamalaki katika jamii zetu hizi.

Tukimsikiliza vizuri Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Samia tutamwelewa anaposema Katiba Mpya ni muhimu. Hivyo ni vema umuhimu huo uanze kukumbatiwa na kuanza angalau na hayo ya INEC na uteuzi huu. **Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Mbunge Makamba ni mfano wa kuigwa kwa utekelezaji ahadi



Na Thobias Mwanakatwe

**Ziara hiyo ambayo ilikuwa kijiji kwa kijiji, hakika mambo mengi aliyoyaahidi amefanikiwa kuyatekeleza hali ambayo kila kijiji alichofika wananchi walimshangilia na kufurahia uwepo wake.**

MBUNGE ni mwakilishi wa wananchi katika bunge. Miongoni mwa majukumu ya mbunge ni pamoja na kutunga sheria na kuwasilisha kero za wananchi wa jimbo lake (wapigakura) kwa serikali ili zipatiwe ufumbuzi.

Ukikuta mbunge ambaye jimbo lake linakabiliwa na kero nyingi hazijatatuliwa, ujue hatekelezi vyema majukumu yake na hii husababisha wapigakura wake kumwadhibu wakati wa uchaguzi mkuu unaofuata.

Kwa mbunge wa Jimbo la Bumbuli, Lushoto mkoani Tanga, January Makamba, suala la kutatua kero za wapigakura wake analipa kipaumbele namba moja na analisimamia vyema na kulitekeleza kwa asilimia kubwa.

Makamba ambaye ni miongoni mwa wabunge vijana na makini katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukifika katika jimbo lake ambalo sasa ni kipindi chake cha tatu kuliongoza, ahadi nyingi alizozitoa wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 amezitekeleza kwa kasi ya ajabu. Hali hiyo inawafanya wapigakura wake kuwa na imani naye kwa asilimia 100.

Mfano hivi karibuni baada ya Bunge la 12 la bajeti kuahirishwa, Makamba alifanya ziara jimboni kwake kwa ajili ya kukagua na kuweka mawe ya msingi miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa.

Ziara hiyo ambayo ilikuwa kijiji kwa kijiji, hakika mambo mengi aliyoyaahidi amefanikiwa kuyatekeleza hali ambayo kila kijiji alichofika wananchi walimshangilia na kufurahia uwepo wake. Hiyo ni tofauti na majimbo mengine ambayo unaweza kukuta mbunge amefika kijijini kuzungumza na wapigakura asilimia kubwa ya wananchi wamenuna.

Mfano wa mambo aliyoahidi na ameyatekeleza ni kuisaidia Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Soni ambayo ilipata janga la mabweni yake kuteketea kwa moto.

Makamba alipofika katika shule hiyo, alitoa msaada wa vitanda 20 vyenye thamani ya Sh. milioni nne, hivyo kukamilisha ahadi yake yote kwa kuwa awali baada ya janga hilo kutokea, alitoa magodoro 100 na mabati 200.

Wakati wa ziara hiyo, Makamba alisema lengo la kusaidia katika shule hiyo ni kutaka kuunga mkono jitihada za kuinua kiwango cha elimu na ufaulu katika jimbo lake. Hatua hiyo ilimfanya apongezwe na uongozi wa shule hiyo chini ya Mkuu wa Shule, Ally Lwena, kwa mbunge huyo kusikia kilio hicho cha vitanda vya wanafunzi wa kike.

Lwena aliweka bayana kwamba kutokana na kukosekana kwa vitanda, wanafunzi walikuwa wakipigwa na baridi kali kutokana na kulala kwenye sakafu na kwamba hali hiyo ilisababisha magonjwa kama vile kukohoa, kubanwa mbavu na vichomi.

Katika suala la miundombinu, Makamba amefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kutokana na jukumu lake la kuwa kiunganishi kati yake na wananchi kwa serilali, ameishawishi serikali ikatoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami na changarawe katika jimbo hilo.

Makamba aliwaeleza wananchi wa kata ya Mponde kuwa atahakikisha anapigania na kulipeleka bungeni suala zima la changamoto ya barabara lililopo maeneo ya vijijini ili kuwapo usawa kati ya mjini na vijijini.

Kuhusu umeme, huko Makamba ndiko kwa kiswahili cha kisasa unaweza kusema amepiga bao. Kati ya kata 18 zilizoko katika jimbo la Bumbuli, 15 zinang'aa kwa umeme, hivyo zimebaki kata tatu tu ambazo ndani ya mwaka huu nazo zitakuwa zimefikiwa na huduma hiyo.

Kimsingi, kwa jinsi Makamba anavyotekeleza ahadi zake katika jimbo hilo, ninasukumwa niseme kuwa huyu ndiye mbunge wa mfano na wa kuigwa.

Nitoe wito kwa wabunge wengine wasisite kuiba mbinu zinazofanywa na Makamba katika kufanikiwa kutatua kero na changamoto zilizopo katika jimbo lake.

Sisemi kuwa kero zimeisha katika jimbo la Bumbuli lakini kwa tunaolijua jimbo hilo lilivyokuwa na lilivyo sasa, hakika linapaa kimaendeleo. Hii ni kutokana na juhudi kubwa zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na Makamba.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA.**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# NAMNA YA KUEPUKA WAKWE NA NDUGU KUINGILIA NDOA - 2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

**Ni busara kufahamu kuwa mtu anapokosana na mke au mume wake, ni vizuri wazazi na ndugu wakawa ndio marafiki zake, hasa kama hawaungi mkono au kupendelea kwenye ugomvi huo kama wanaufahamu.**

WIKI kadhaa zilizopita tuliangalia baadhi ya mambo yanayosababisha ndugu na wazazi au wakwe kuingilia ndoa na hatimaye kusababisha wanandoa washindwe kuchukua hatua kunusuru ndoa pale tatizo linapojitokeza.

Lakini wiki iliyopita, tuliangalia namna wanandoa wanavyokwepa kihunzi na kikwazo hicho cha ustawi wa ndoa yao. Miongoni mwa njia hizo ni kuepuka upendeleo na kubadili mitazamo potofu.

Sehemu hii ya pili na ya mwisho inaelezea njia zingine, licha ya kwamba si zote katika kuhakikisha wanandoa wanakwepa kuingiliwa kwenye ndoa yao. Baadhi ya njia hizo ni;-

### Epuka chuki

Mara baada ya ndoa wazazi au ndugu nao huanza kufanya ubaya. Uadui unakuwa umeanza. Ni busara kufahamu kuwa mtu anapokosana na mke au mume wake, ni vizuri wazazi na ndugu wakawa ndio marafiki zake, hasa kama hawaungi mkono au kupendelea kwenye ugomvi huo kama wanaufahamu. Kinyume na hapo, hata mtu anapokuja kuelewana na mume au mke wake bado wazazi na ndugu zake watakuwa na uadui naye.

### Epuka kulinganisha familia

Kuna wakati mume na mke wanajikuta wanabishana kuhusu familia zao. Inaweza ikawa ni ubishi kuhusu familia ya nani ina uwezo, ina heshima, ina upendo na mengine ya aina hiyo. Hili ni jambo la hatari kwa sababu yule ambaye ataona ameshindwa, ataanza polepole kujihisi mnyonge kifamilia na uwezekano wa kuanza kuichukia familia ya mwenzake utakuwa mkubwa pia.

Ni vizuri wanandoa wakachukulia kwamba kila familia ya mwenzake ni bora kama yake hata kama kuna kasoro na tofauti kubwa. Ikumbukwe kuwa watu wanapooana wanakuwa ni mwili mmoja, Kikristo. Hivyo, wazazi na ndugu zao wanahusika sawa kwenye mwili huo, lakini si kuingilia ndoa.

Usitende usiyopenda kutendewa

Kumbuka unavyowafanyia wengine ndivyo ambavyo nao watakufanyia. Hivyo, ukiona mtu anakuudhi, anakuchukia, anakukera, anakukebehi, jiulize kama nawe humtendei mambo ya aina hiyo. Ukiwapenda wengine, nawe watakupenda. Ukiwachukia na kuwatendea ubaya, itakuwa hivyo hivyo kwako.

Usisubiri mtu aanze kukupenda wewe, kwani hilo siyo lazima lifanyike, kwa sababu huenda naye ni kama wewe, anasubiri uanze kumpenda kwanza. Ni vyema sisi tukawa ndio tunaoanza kuwapenda wengine. Kuwapenda huku kusiwe kwa masharti, kwani kupenda kwa namna hiyo si kupenda bali na aina ya biashara.

Tuwapende tu bila kujali kama wao wanatupenda au kutufanyia kama tunavyowafanyia wao. Kupenda iwe ni tabia yetu na sio huduma kwa watu, wakati na mahali maalumu.

Si kwa wakwe au ndugu, bali kwa binadamu wote. Tukijifunza kuacha chuki na badala yake tukajifunza kufurahia mafanikio ya wengine, tukawakubali wengine kama walivyo na kuwavumilia, tutaishi vizuri na kila mtu.

Kuwakubali kama walivyo maana yake ni kuwapenda.Tukiwapenda maana yake na wao watatupenda pia. Hebu wapende kwa nguvu zote, wakwe, mawifi au mashemeji zako wakorofi, halafu subiri matokeo yake. Bila shaka matokeo ni furaha. Jifanye kama vile unajua kwamba watakufa wiki ijayo, hivyo wape upendo wa mwisho.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

Agosti 8, 2021

Nipashe Jumapili

Baba, Mama na Mwana


Ukurasa 15



## MAISHA NI NYUMBA

### Umuhimu wa ukuta katika kufanya nyumba kuwa bora



## Usiku wa Esta

**FAMILIA YA ODWIN MWANSASU WAMBALIZI ILIPOMUAGA BINTI YAO KIPENZI ESTA KWA SHEREHE ILIYOFANA SANA KATIKA UKUMBI WA TUGHIMBE JIJINI MBEYA**

**SENDOFF**

Tunachapicha picha za harusi bure wasiliana kwa namba

Ukurasa 12

## FURAHIA JUISI YA UBUYU





Ukurasa 14





# NYWELE ASILI ZINAVYONG'ARISHA WAREMBO

Ukurasa 13








## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
TIA, ALA, AKA, ADI, RELI, KABA, FAHARI, AKHERA

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



SWALI
Taja faida ya mito ya asili

MTOTO mmoja alitaka kujua kile anachofundishwa kama kina usahihi, aliporudi nyumbani alianza kumuuliza mama yake maswali.

Mtoto: Mama hivi mvua inatoka wapi?

Mama: Inatoka mbinguni

Mtoto: Kwani mvua inakwenda kujisaidia?

Mama: Hapana inanyesha tu

Mtoto: Mbona shuleni tumejifunza kwamba asifiaye mvua imemnyea?

Mama: Hiyo ni msemo tu, una maana nyingi

Mtoto: Duuh! Mi nilijua tofauti

# MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



## Jukumu la kulinda ulicho nacho ni lako mwenyewe

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki mbili zilizopita nilijadili aina mbili za wanawake wanaotikisa ndoa zao kiasi cha kuwafanya wanaume wawe na taharuki ya kimaisha.

Mwanamke wa kwanza alikuwa hajali watoto, akienda kwenye kazi yake ya ufundi cherehani hurudi usiku huku watoto wakisubiri nje ya nyumba baada ya kurejea kutoka shuleni.

Mume akagundua kuwa yuko mwanamume wa nje anayemzuzua mkewe na ndiye anayemchelewesha kurudi nyumbani. Mzozo wa ndoa hii uko katika hatua za usuluhishi.

Pia nikatoa mfano wa mwanamke mwingine ambaye huyu ni hodari sana wa kumpiga mumewe. Wanandoa hawa ni wanywaji wa pombe na mara nyingi mzozo ni mkali wakisha kunywa.

Mke huyu pia amekuwa akimsimanga mumewe kwa anachodai hajachangia sehemu kubwa ya fedha zilizojenga nyumba wanayoishi. Suluba zote hizo zimemuumiza mwanamume kiasi kwamba hivi sasa anajiandaa kutafuta makazi salama atengane na mkewe.

Mpenzi msomaji, nimekumbushia mifano hiyo miwili ili sasa nieleze siri ya kuondokana na kadhia za aina hiyo.

Nimeeleza mara nyingi hapa kwamba hakuna jambo linalotokea kwa bahati mbaya kwani lazima kiwapo chanzo chake.

Mwanamke wa kwanza niliyemwelezea hapo juu chanzo cha kutikisika ndoa yake ni yule mchepuko aliyemnasa, hivyo kumchelewesha kurudi mapema kuhudumia familia yake. Huyo wa pili ni kilevi, kumpiga na kumsimanga mumewe pasipo sababu yenye mashiko.

Watu wengi wamejikuta katika mitikisiko ya ndoa pasipo kujua siri zilizojificha ambazo zingeweza kuepusha yale wanayopitia. Kikubwa ni kutunza kile ambacho Mungu amekupa kuendeleza maisha.

Ni vyema ukaelewa kwamba chochote ulichopewa ni mali yako. Safari ya maisha ni vita. Kuna wakati utapanda milima na kuna wakati utapata kitu kizuri kikaibwa. Hata Mungu katika moja ya maandiko yake anasema: "Linda sana ulicho nacho asije mtu akatwaa taji yako."

Ukishapewa kitu, jukumu lako ni kukilinda, kukitunza. Usipokuwa makini katika eneo hilo, kuibiwa ni lazima. Hata mafanikio huibwa. Unaweza ukawa na mafanikio makubwa kiuchumi, wakajitokeza watu wabaya wakakuvuruga, wakakulaghai ukaporomoka ukajikuta chini.

Chochote kilicho chako lazima ukipiganie. Nafasi nzuri inalindwa kwa gharama zote. Kama ni mume, mke mlinde.

Mtu anaweza kuulinza; Tunalinda nini? Kwanza tunalinda hatua za mafanikio ili tufike kule ambako Mungu anataka tufike kimaisha. Vilevile tunalinda vipawa na karama (vipaji) alivyotupatia Mungu. Kile kitu unachoweza kufanya kuliko wengine, hicho ni kipawa.

Tunapaswa pia kulinda mafanikio yetu. Shetani anafanya kazi pande mbili; ulimwengu wa roho na ulimwengu wa mwili. Unapoanza kupata mafanikio ndipo maadui huinuka. Unapopata kitu kizuri ndipo shetani huja. Tulinde sana vile vitu Mungu ametupatia iwe ni kazi, familia vinginevyo adui atachukua.

Ni rahisi watu au marafiki kukutia moyo pale unapoinuka, lakini ukiporomoka watakukimbia. Pia kuwa makini na watu wabaya kwani wakati mwingine huja kwako kuchukua kile ulicho nacho. Wengi wamehaibiwa ndoa na marafiki, majirani na kadhalika. Ni muhimu umwombe sana Mungu akulindie kile ulicho nacho.

Mpenzi msomaji, hebu pia jiulize, Je, ni kwa nini mtu anapewa halafu anapoteza? Moja ya sababu ni kuvunjwa moyo au kukatishwa tamaa. Tabia mbaya ya mke au mume yaweza kumkatisha tamaa mmojawapo na ndoa ikavunjika. Unahitaji watu wa kukutia moyo na pia kukuinua ili usonge mbele. Usikubali kukata tamaa kirahisi. Pia uwe na tahadhari kwamba ukiwa na kitu kizuri, siyo kila mtu umwambie, tunza siri zako. Mawazo yako mazuri yaweza kudakwa na wenzio, wakayafanyia kazi, wakafanikiwa na wewe ukabakia vilevile.

Wako watu waliowasifia wake au waume hadharani na leo hii wanalia nyumba hazikaliki, kisa walitoa siri za ndoa zao. Eti mke wangu ni mzuri sana, ana tabia nzuri, anajua kupika, anavaa vizuri. Lo! Kumbe unaowaeleza ni maadui wanakutega wakuibie mkeo!

Wengine wameshindwa kulinda vizuri walivyopewa na Mungu kwa kujilinganisha na mtu mwingine. Kumbuka, jinsi ulivyo hufanani na mwingine. Mungu amekuumba kwa jinsi yako na kwa utukufu wake. Maisha yako usiyalinganishe na ya mwingine.

Si kila njia ya mwenzio iwe njia yako. Pia linda ulicho nacho kikuvushe kimaisha. Hadi wiki ijayo. Una maoni tuma 0715268581.

# NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



## Elimu ya chanjo iendelee kutolewa kuokoa maisha ya wengi

JULAI 28, mwaka huu, Tanzania iliungana na nchi zingine duniani kuanza kutoa chanjo ya corona kwa wananchi wake ikiwa ni hiari ya mpokeaji.

Chanjo hiyo imeendelea kusambazwa sehemu mbalimbali na wanaohitaji wanachanja, lakini wengi bado wanajiuliza maswali mengi na huku taarifa potofu zikishika kasi huku zikichagizwa na viongozi ambao wana wafuasi wengi kwenye jamii.

Cha kueleweka na muhimu ni kila mtu atambue kuwa afya ni suala binafsi na uamuzi wa kuchanja au kutokuchanja pia ni binafsi, asishawishiwe bali atafate taarifa sahihi kwa watu sahihi.

Baadhi ya maeneo watu wameacha kuchanja kwa sababu wameambiwa watapata madhara lakini wanasahau hatari kubwa iliyo mbele yao ikiwa hawatakubali kuchanja.

Maneno ya mtaani ni mengi na hapo ndipo wajibu wa wataalam wa afya unapotakiwa kudhihirika kwamba elimu sahihi itolewe na watu sahihi kwa wakati sahihi ili wanachi wafanye uamuzi sahihi.

Elimu ianze kwa wataalam wenyewe, wapikwe kwanza na kuelewa ili wapeleke elimu sahihi. Mathalani  wale wanaohusika kuchanja wanapoulizwa maswali waweze kujibu ili kuepusha watu kuchanjwa pasipokujibiwa maswahi yote muhimu.

Kwa mfano, nilipokwenda kuchanja niliuliza maswali kadhaa ambayo aliyekuwa anatoa chanjo hakuwa na jibu kiasi cha kujiuliza, je, ni kwamba hajui au kimya chake kinamaanisha nini?

Swali ni kama mtu ana mzio (allergy fulani anaruhusiwa kuchanjwa? Wajawazito je, nao wanaruhusiwa? Je, mtu aliyekunywa pombe siku ya kuamkia chanjo anaruhusiwa? Je, ambaye ni mgonjwa wa magonjwa sugu au mengine?

Kwa ujumla hakukua na jibu na hata elimu bado haijatolewa na haya ni maswali mengi yanayosubiri majibu kutoka kwa watu sahihi ambao sasa wanapaswa kuwayajibu.

Hakuna ubishi kuwa awali ilikuwa nguvu kwa mwananchi yeyote kuzungumzia suala la UVIKO 19, ila sasa linazungumziwa kwa uwazi na yeyote anayeugua anasema hata anapofariki madaktari wanasema kwa uwazi.

Kwa msingi huo sasa tuone wataalam wakitumia vyombo vya habari kuelimisha umma, wakitoa machapisho yasambazwe maeneo yote hata vijijini ili wananchi watambue nini haswa maana ya ugonjwa na hatua za kuchukua.

UVUKO 19 itaendelea kuwepo na tutaishi nao, na mbaya ni kuwa kila mara kirusi kinajibadili umbo kiasi cha kuwa na dalili mpya na namna mpya ya kutibu, huku wanasayansi wakiumiza vichwa namna ya kukabiliana nacho.

Kama ambavyo serikali imesema italeta chanjo nyingine ili wananchi wengi zaidi wachanje maana yake elimu sahihi itawezesha wengi kupata chanjo na kupunguza idadi ya wagonjwa mahututi na vifo.

Tayari Marekani imesema asilimia 90 ya vifo vya UVIKO 19 kwa sasa nchini humo ni vya wale ambao hawakukubali kuchanjwa, maana yake ikiwa wengi watachanjwa basi watapunguza hatari ya kufa au hospitali kujaza wagonjwa.

Ni muhimu viongozi wa dini wenye kuamini kwenye sayansi ambao wamesoma na kujiridhisha namna chanjo ni salama, wakawaambia waumini wao umuhimu huo kwa kuwa chanjo imeanza kuhusishwa na masuala ya kiimani.

Ziko nchi zimefanikiwa baada ya kuchanja watu wake na sasa shughuli zinaendelea kama kawaida na wataalam wa afya ambao ndiyo askari wa mwavuli wanaotangulia mbele hawajaelemewa na wagonjwa kiasi cha kuwagharimu na kuigharimu serikali.

Dhana nyingi zinazoelezwa ni muhimu zikafafanuliwa vyema kwa wananchi na kuunganisha nguvu kubwa kwa kuwa uongo ukiachwa ukasemwa sana utavikwa vazi la ukweli jambo ambalo si sahihi kabisa.

Ni muhimu machapisho na vipeperushi vikabandikwa kwenye ofisi za serikali za mitaa, vijiji, kata, tarafa, wilaya, halmashauri na kwingine kote na maeneo yenye kuwakusanya wananchi wengi ikiwamo mipakani.

Mungu ibariki Tanzania.

# Usiku wa Esta

**FAMILIA YA ODWIN MWANSASU YA MBALIZI ILIPOMUAGA BINTI YAO KIPENZI ESTA KWA SHEREHE ILIYOFANA SANA KATIKA UKUMBI WA TUGHIMBE, JIJINI MBEYA**












Tunachapicha picha za harusi bure wasiliana kwa namba 0717336368, au barua pepe: Moshilusonzo@Gmail.com"
Moshilusonzo@Gmail.com.

# MITINDO

## VAA BARAKOA JILINDE NA UPENDEZE



KUFUATIA janga la virusi vya Corona, serikali imetangaza kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa huo. Pamoja na kuanza utoaji chanjo kwa makundi ya watu, pia imehimiza matumizi ya barakoa kama njia sahihi ya kulinda dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo.

Baadhi ya watu ambao wanapenda umaridadi wanakuwa na wasiwasi kuhusu kutumia barakoa zilizotengenezwa viwandani, lakini umepewa nafasi ya kununua zile zinazotengenezwa na wabunifu.

Kutokana na chaguo hilo, barakoa yako itakuwa sit u kifaa cha kulinda, bali ni moja ya vazi linaloweza kukupa utofauti na wengine.

Wataalamu wa mavazi wanasema kama unataka kutoka vizuri, basi unaweza kutengeneza barakoa inayofanana na moja ya nguo zako kama suruali au shati na ukavaa kwa wakati mmoja.

Hakikisha kitambaa cha nje ya barakoa kiwe kinafanana na vazi lako na iwe imekaa vyema kutoka chini ya kidevu hadi mwisho wa pua.

Tazama baadhi ya picha zinazoonyesha jinsi barakoa zilizobuniwa vizuri zinapovaliwa.



URBEMBO: ZIMEBAMBA MITAANI

# Nywele asili zinavyong'arisha warembo



NYWELE ni sehemu kubwa ya utanashati na urembo katika mwonekano mzima wa mwanamke.

Mwanamke ili uvutie na kupendeza katika vazi ulilolipigilia unapaswa kuzingatia usafi wa nywele yako.

Utunzaji wa nywele za asili kwa sasa umeshika kasi nchini na kufanya kuibuka kwa mitindo mbalimbali inayovutia.

**UTUNZAJI NYWELE ASILI**

Jambo zuri kama utaonekana asilia na mng'aro unaovutia, katika kufanikisha hili hakikisha unaziosha nywele zako na kubadili mtindo wa kubana kila baada ya wiki mbili.

Nywele za asili hazina kazi katika utunzaji wake na zinampa uhuru mtu kuziweka katika mtindo anaoutaka.

Wale ambao wanapenda kuzibana nywele, ni lazima kuwa waangalifu kwa kuziosha kwa maji ya vuguvugu mara kwa mara ili ziwe safi.

Baada ya kuzikausha unaweza sasa kuzipaka mafuta ya nywele yatokanayo na mbegu za asili kama nazi, mnyonyo, mawese, parachichi na mzaituni.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# FURAHIA JUISI YA UBUYU



MBUYU ni miongoni mwa miti yenye faida nyingi na maajabu mengi. Vitu vyote vilivyomo kwenye mbuyu vinatumika kama chakula au dawa kwa faida ya binadamu.

Juisi ya Ubuyu

Unga wa ubuyu unaelezwa kuwa na vitamini na madini mengi kuliko matunda mengine yoyote likiwamo chungwa.

Juisi ya ubuyu inatengenezwa kwa kuchemsha maji ya moto lita mbili, ukishaepua mimina unga wa ubuyu nusu kilo na acha mpaka upoe.

Chuja juisi yako na uongeze sukari kiasi, iweke kwenye friji na itakuwa tayari kwa matumizi ya familia.

faida za juisi ya ubuyu

Unga wa ubuyu una vitamini C mara sita zaidi ya ile inayopatikana katika machungwa, una madini ya Kashiamu mara mbili zaidi ya maziwa ya ng'ombe na pamoja na madini ya Chuma, Magnesiamu na Potasiamu ambayo ni mara sita zaidi ya ile potasiamu ipatikanayo katika ndizi.

Juisi ya ubuyu husaidia kujenga neva za fahamu mwilini na ina virutubisho vya kulinda mwili.

Ubuyu una vitamini B3 na B2 ambayo ni muhimu katika kuondoa sumu mwilini na umeng'enyaji wa madini ya chuma, kimsingi vyakula vyenye afya zaidi kwa ajili ya mwili ya binadamu huwa na vitamin B2.

Juisi ya ubuyu inaongeza kinga ya mwili sababu ya kuwa na kiasi kingi cha vitamini C, huongeza nuru ya macho, husaidia kuzuia kuharisha na kutapika, ina magnesiamu ambayo husaidia kujenga mifupa na meno na husaidia wenye presha ya kushuka na wenye matatizo ya figo.

Jipatie kikombe kimoja cha juisi ya ubuyu kila siku hasa usiku na baada ya wiki kadhaa utaona matokeo ya mwili.

Ubuyu mzuri kutumiwa ni ule mweupe usiochanganywa na kitu kingine cha kuongeza ladha au rangi.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## UMUHIMU WA UKUTA KATIKA KUFANYA NYUMBA KUWA BORA



KUNA mambo mengi ambayo huchangia kuleta athari kwenye nyumba na hili tumekuwa tukijifunza kutoka katika maelezo ya wataalam mbalimbali kutoka kwenye sekta hiyo.

UKUTA wa nyumba ni sehemu muhimu na ya kudumu na ndiyo hushikilia ustawi na uimara wa nyumba au jengo lolote.

Mara nyingine matokeo ya nyumba nzuri na uimara wake huonekana kwa nje ikiwa imenakshiwa vizuri bila kujua siri ya vitu gani vilivyotumika mpaka kufikia kuonekana katika hali hiyo.

Mtaalam wa ujenzi, Victor Mkalama, anasema ukuta anaozungumzia ni ule ambao hutokana na mchanganyiko wa zege au mawe na kufanyiwa utaalam wa uashi na kusimama kama ukuta ambao baadaye huitwa nyumba.

Anasema jambo la msingi la kufahamu katika kutambua kama unataka kuwa na ukuta wa nyumba bora, imara na wa kudumu unatakiwa kuhakikisha unakuwa makini na aina ya malighafi unayotumia ambayo inaendana na mazingira ya eneo husika.

Jambo lingine anasema la kuzingatia ni mtindo na muundo wa nyumba husika

"Na katika hili unapaswa kufahamu pia kwamba nyumba unayojenga ni ya mtindo na ya muundo gani na pia kama ni wa kutumia mawe au matofali ili fundi anayejenga akushauri kutokana na mazingira ya eneo lako," anasema Mkalama.

Anaongeza kuwa: "Ukuta bora, imara na ambao ni wa kudumu unategemea sana na aina ya malighafi. Ikumbukwe kwamba ukuta wa tope, mawe au tofali ubora na uimara wake hutofautiana sana, na ndiyo maana tunashauri sana kupata ushauri kutoka kwa wataalam.

"Kwa hiyo hata katika ufundi katika kujenga nyumba yenye ukuta bora hakuwezi kutokana na ubunifu pekee kutoka kwa fundi unategemeana sana. Hivyo vitu vitatu ambavyo ni malighafi, mazingira ya eneo ambalo nyumba husika inajengwa na muundo wake, halafu ufundi ni wa mwisho."

Pia anasema katika kazi ya kujenga ukuta wa nyumba au wa jengo lolote ni lazima kuzingatia uzito unaoendana na jengo husika.

"Ukuta usioendana na aina ya jengo unaweza kuleta shida kwenye jengo au nyumba baadae. Na aina ya kwanza ya ukuta unaobeba uzito wa jengo hujengwa kwa kutumia tofali za kuchoma, mawe au tofali za zege/mchanga."

"Kazi ya ukuta wa aina hii hufanya kazi kubwa ya kuchukua na kusafirisha uzito wa paa au jengo hata kama ni nyumba ya kawaida au ghorofa," anasisitiza.

# MPANGILIO

## UNATAKA KUPAMBA SEBULE AU BAFU KWA KUTUMIA MISHUMAA? BASI HIZI NI BAADHI YA DONDOO MUHIMU ZA KUPAMBA ILI KUWEKA MANDHARI NZURI USIKU

1: Vibakuli au glasi vyenye mishumaa inapendeza katika meza ya chakula, pamoja na mwanga pia inaleta mandhari ya kupendeza.


2: Mishumaa mikubwa yenye kibebeo chake maalumu, inapendeza kuweka katika pembe ya nyumba au bafuni kwani inaleta taswira nzuri na mwanga unaovutia.

3: Mishumaa inayoelea inapendeza kupamba sebule, chukua chombo chenye maji na kisha weka mishumaa katika kibebeo kinachoelea, mwanga wake unapoakisi maji inaleta mandhari ya kuvutia.

4: Mishumaa iliyowekwa katika chupa iliyolazwa inapendeza sana, ni muhimu wakati mshumaa unawaka weka maua pembeni ili kunogesha zaidi.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...KILA WIMBO NA UCHEZAJI WAKE

## HABARI KIMATAIFA

# Taliban wazidi kusonga mbele washika miji kuelekea Kabul

**ABUL,** AFAGHANSTAN

WANAMGAMBO wa itikadi kali wa Taliban, wameukamata mji wa Sheberghan katika mkoa wa Jawzjan, ukiwa ni mji mkuu wa pili kuangukia mikononi mwao.

Naibu Gavana wa mkoa huo, Qader Malia, alisema jana kuwa wanajeshi wa serikali na maofisa wamekimbilia uwanja wa ndege.

Mji huo ni nyumbani kwa mbabe wa kivita, Abdul Rashid Dostun, ambaye alirejea nchini humo wiki hii akitokea Uturuki alikokuwa akitibiwa.

Taliban waliutwaa mji mkuu wa mkoa wa Nimroz ulioko Mkoa wa Zaranj siku ya Alhamisi.

Naibu gavana wa mkoa huo uliopo kusini magharibi , Roh Khairzad, alisema mji huo unaopakana na Iran unashikiliwa na wanamgambo hao.

Alisema mji huo ulikamatwa bila ya mapambano yoyote. Msemaji wa Taliban, alisema wanamgambo wamechukua udhibiti wa nyumba ya gavana, makao makuu ya polisi na majengo mengine ya serikali.

Mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Afghanistan, Deborah Lyons, ametoa wito kwa kundi la Taliban kusitisha mara moja mashambulizi yake kwenye miji mikuu, huku akionya kuwa mgogoro huo unelekea kuwa janga.

**DW.**



Waendesha mkokoteni wakimvusha abiria wao baada ya mafuriko kuukumba mji wa Navotas city, katika Jimbo la Metro Manila, nchini Philippines juzi. **PICHA EPA**

# Moto wazidi kuziangamiza Uturuki, Ugiriki

**ATHENS,** UGIRIKI

MOTO wa msituni unaendelea kuteketeza maeneo makubwa yaliyobaki katika misitu ya Ugiriki na kuyafikia maeneo ya makazi ya watu.

Kulingana na taarifa kuhusu janga hilo, moto huo baada ya kuharibu nyumba, biashara na mashamba, sasa unaelekea katika miji ambayo inakaliwa na watu wengi. Katika nchi jirani ya Uturuki, moto ulioelezwa kuwa mbaya zaidi kuwahi kushuhudiwa katika miongo mingi, umeteketeza maeneo ya pwani ya kusini mwa nchi hiyo kwa siku kumi, na watu wanane wamefariki dunia. Askari mmoja wa zima moto wa kujitolea amefariki jana, wakati wengine 20 wakijeruhiwa baada ya moto huo kuiteketeza sehemu kubwa ya mbuga ya taifa katika mji mkuu wa Ugiriki, Athens.

Maelfu ya wakazi na watalii walikimbia kwa kutumia magari na boti.

Vikosi vya zima moto na ndege vimewasili nchini humo kutoka Ufaransa, Ukraine, Cyprus, Croatia, Sweden na Isrel, huku waokoaji zaidi vikitarajiwa kuwasili jana kutoka Romania na Uswisi.

**DW**

# Marekani yawawekea vikwazo viongozi wa wanamgambo

**WASHINGTON,** MAREKANI

SERIKALI ya Marekani imeongeza vikwazo kwa wanachama watano waandamizi wa makundi ya itikadi kali barani Afrika.

Kwenye orodha hiyo iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje, imeeleza watu hao watazuiliwa mali zao na maslahi yoyote waliyonayo nchini Marekani.

Vikwazo hivyo vitamgusa Bonomade Machude Omar, kamanda mwandamizi wa kundi la Dola la Kiislamu (IS) linalopigana nchini Msumbuji, ambaye aliongoza shambulizi kwenye hoteli ya Amarula mjini Palma Machi, mwaka huu.

Taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ilisema Omar pia alihusika na mashambulizi mengine nchini Msumbiji na Tanzania.

Wengine waliowekwa kwenye orodha hiyo ni Sidan ag Hitta na Salem ould Breihmarr, ambao ni viongozi waandamizi wa tawi la Al-Qaeda nchini Mali la Jama'at Nasr al-Islam wal Muslimin (JNIM).

Aidha, watu wengine ni Ali Mohamed Rage, msemaji wa kundi la al-Shabaab, na Abdikadir Mohamed Abdikadir, anayesimamia mipango ya operesheni za kundi hilo.

**DW.**

## Waasi waua 15 Beni

**GOMA,** CONGO DRC

WATU 15 wameuawa kwenye mashambulizi ya siku mbili yanayohusishwa na waasi wa itikadi kali karibu na mji wa Beni, katika eneo la mashariki mwa Congo.

Mkuu wa shirika la kiraia katika mji jirani wa Mamove, Kinos Kathuho, alisema shambulizi la kwanza lilisababisha vifo vya watu kumi, wakiwamo wanawake watano katika kijiji cha Mbingi.Watu wanne walijeruhiwa.

Shambulizi la pili, lilitokea juzi asubuhi, katika Kijiji cha Mapasana, kilomita moja tu kutoka lilikofanyika la kwanza na kusababisha vifo vya watu watano.

Kiongozi wa eneo hilo Omar Kalisya, alisema pamoja na mauaji hayo, pia waliwaacha watu kadhaa wakiwa wamejeruhiwa na wengine hawajulikani walipo.

Katika tukio hilo, nyumba zilichomwa moto na maduka kuporwa.

Katika matukio yote, wahanga walikatwa kwa mapanga au kupigwa risasi hadi kufa, huku taarifa zinaeleza mashambulio hayo yalifanywa na waasi wa ADF.

**DW.**

## Ethiopia yatishia kuivamia tena Tigray

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

ETHIOPIA imeonya kuwa huenda ikapeleka nguvu zake za kijeshi baada ya waasi wa Tigray kuendeleza mashambulizi yao mikoa jirani.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje, ilisema serikali inasukumwa kukusanya uwezo wake wa kijeshi kama juhudi zake za kibinadamu za kutafuta ufumbuzi wa amani katika mzozo huo hazitazingatiwa.

Juzi, msemaji wa Jeshi la Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPL), alikataa miito ya kuwataka waondoke katika maeneo jirani ya Afar na Amhara.

Matamshi hayo yamekuja siku moja baada ya waasi kukamata eneo la Lalibela, ambalo ni sehemu ya Turathi za Ulimwengu katika Mkoa wa Amhara.

Waziri Mkuu Abiy Ahmed, alitangaza usitishwaji mapigano mwishoni mwa Juni, mwaka huu, baada ya wanajeshi wa TPLF kukamata tena mji mkuu wa Tigray, Mekelle.

**DW.**

## MAKALA

# TUWATHAMINI WATAKUWA WAZALENDO



Na Magabilo Masambu

SHULENI wanafunzi wanapofanya mtihani, mwalimu huweka alama ya vema au kosa. Alama hizo si tu kazi yake ni kuonyesha kwamba mwanafunzi amekosea au amepatia swali, bali ni kutambua na kuthamini kazi yake aliyoifanya.

Ndiyo maana mtoto mdogo akikosea swali ili kumjengea morali ya kupenda kufanya kazi yake ya shule, si busara kuweka alama kubwa ya kosa. Unapaswa kumwekea alama ndogo sana ya kosa na pale anapofanya vizuri umwekee alama kubwa ya vema.

Alama kubwa ya vema inamfanya aone na aamini kwamba anaweza kufanya vizuri zaidi, hivyo kila akifanya swali atataka umwekee alama ya vema. Kwa hiyo atajitahidi kufanya vizuri kila siku ili aipate. Uzalendo utajengeka miongoni mwa watu wetu pale tu kila mtu katika taifa atakapothaminiwa na kuona anayo fursa ya kutoa mchango wake katika maendeleo ya nchi yake.

Siku moja nimewahi kusikia mzee mmoja akimwambia kijana wake: "Kama hutaki shule acha, maana elimu wala ajira yako havitanihusu kwa lolote." Mzee alisema hivyo kwa kuwa bado alikuwa na kazi nzuri na ana nguvu za kufanya kazi bado lakini alisahau kuwa hajui ataishi miaka mingapi. Maana hata kama atakuwa na kazi nzuri kiasi gani, iko siku hatakuwa na uwezo wa kufanya kazi tena kutokana na uzee au ugonjwa na pengine akafikia umri ambao hata macho yake hayatakuwa na uwezo wa kuona tena.

Kwa hiyo anapomsomesha kijana wake kwa upande mwingine, pamoja na kwamba anaandaa maisha ya kijana huyo, anamwandaa pia aje amtunze pindi atakapokuwa hana nguvu tena za kufanya kazi. Vivyo hivyo kwa taifa, pamoja na kwamba kila raia anao wajibu wa kulinda nchi yake, lazima uwapo utaratibu unaowapa wananchi motisha na morali kubwa ya kulinda mali na rasilimali za taifa lao kama sehemu ya kuthamini mchango wao.

Leo hii tuna wataalamu wengi kutoka Afrika, ambao wanatumiwa kujenga uchumi katika mataifa mengine nje wakati hapa kwetu hawapewi nafasi na kipaumbele katika kuthaminiwa ili waonyeshe uwezo wao. Pengine tuamini kwamba "Nabii hakubaliki kwao". Kushindwa kuwathamini watu wetu ni sawa na kuwekeza mbegu za mpunga kwenye mawe yasiyo na udongo.

Tunawalipa wageni pesa nyingi kwa kazi ambazo wanaweza kufanya watu wetu. Ujuzi haujengwi vitabuni bali hujengwa kazini ndiyo maana Waingereza wanasema "Practice makes perfect".

Eneo la michezo kwenye timu zetu, tumekuwa na imani kwamba ili timu iwe ya maana ni kuwa na kocha mgeni huku tukiwa na makocha wengi wazalendo wa Afrika hawana kazi! Ukiuliza unaambiwa kuwa hawana uzoefu.

Hivi watapataje uzoefu bila kuwapatia kazi? Watakuwaje wazalendo na wajuzi kama wataendelea kuwa chini ya wageni? Leo hii tunaona fahari sana kuwa na timu yenye wachezaji karibu asilimia 85 kutoka nje. Kwenye mashindano tukishinda tunajisifu kuwa tuna timu bora na kwamba tumeshinda! Hii ni aibu kubwa.

Kama ni timu tufundishe vijana wetu. Masuala ya kutolea mifano kwamba mbona timu fulani ya Ulaya nayo inakodisha wachezaji, tuachane na kauli dhaifu kama hizo. Tunajidhalilisha na ni fedheha kwetu. Kama ni makocha tufundishe wa kwetu na tuwapatie kazi watajifunza tusifanye utatuzi wa mambo kwa muda mfupi wakati tunasababisha matatizo ya muda mrefu. Jambo hili si kwamba tu linaonyesha kuwa tumekuwa dhaifu bali bado linadhalilisha utu wetu.

Hatutaishia kuajiri makocha wa kigeni tu bali hata idara nyeti kama afya, madaktari bingwa wataendelea kutoka nje ya nchi, hata wakiwa ni wanafunzi wa maprofesa wetu mradi wanatoka India, Ujerumani, Australia na kwingineko huku tukiwasomesha wa kwetu hapa kisha kuwaweka kwenye makapu.

Ni ukweli kwamba toka awamu ya kwanza hadi leo awamu ya sita ya utawala wa Tanzania, pamekuwapo na maendeleo makubwa hasa katika sekta ya ujenzi na usafirishaji, ambapo miundombinu kama vile madaraja na barabara vimejengwa na vinaendelea kupanuliwa na kurekebishwa.

Waliofanya kazi hiyo na wanaoendelea kujenga kwa sehemu kubwa ni wahandisi wa kigeni. Hao ndio hupewa tenda hizo kana kwamba vyuo vikuu vyetu havijawahi kutoa wahitimu katika fani hizo miaka 60 tangu tupate uhuru. Kwa hiyo tuliposema kwaheri ukoloni tulimaanisha pia kwaheri uhuru!

Tumebaki kusema wasomi wetu hawana ujuzi, watakuwaje na ujuzi kama hawapewi kazi? Mara kadhaa tumesikia kwamba lazima awe na uzoefu wa miaka isiyopungua mitano ebo! Sasa shuleni kuna uzoefu au uzoefu unapatikana kazini? Mtoto wa watu katoka chuo unataka uzoefu autoe wapi?

Haiwezekani taifa lisomeshe watu, halafu lisiwaamini. Ili mtu awe mzalendo sharti kwanza aaminiwe na pili athaminiwe ili afanye kazi ya kujenga taifa lake kwa moyo wake wote, huku akiamini kuwa faida yoyote itakayopatikana ni kwa ajili ya watu wote na si kwa ajili ya watu wachache tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Balisidya alipotaka kuipindua Dar Jazz



Na Adam Fungamwango

KWENYE tasnia ya muziki wa dansi, hasa wa zamani kuna hadithi nyingi sana zinazozungumzwa, zilizozungumzwa, lakini pia kuna zile ambazo hazijazungumzwa.

Pamoja na mashabiki wa muziki wa dansi hasa ule ya miaka ya 1960 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 kusikiliza na kufurahia muziki huo, bado kuna mambo mengi ambayo yamepitika na bado watu hawakuyajua.

Kwa sasa angalau mashabiki wamekuwa wakisikia maelezo mengi kama vile muziki fulani ulipigwa kwa madhumuni gani. Lakini inavyoonekana muziki huo bado una hadithi nyingi ambazo zitaendelea kuibuka vizazi kwa vizazi.

Labda wakati huo watu walikuwa hawajui kwa sababu hakukuwa na vyombo vingi vya habari na mitandao ya kijamii. Kukosekana kwa wachambuzi siku za nyuma ambao wangekuwa na uwezo wa kudodosa hili na lile, nalo liliwanyima nafasi mashabiki kujua vitu vingi. Kwa sasa kuna habari na hadithi nyingi zinajitokeza na kuzungumza hadi mtu unashangaa.

Mfano, bendi ya Bana Ngenge ambayo ilitisha sana miaka ya 1980 nchini Kenya, kumbe ilikuwa nchini Tanzania na kulazimika kukimbilia nchini humo kwa kuikimbia Orchestra Safari Sound chini ya mtindo wa 'Masantula Ngoma ya Mpwita' ikiongozwa na Kikumbi Mwanza Mpango, maarufu kama King Kiki.

Mmoja wa wanamuziki wa OSS, hivi karibuni alikaririwa kwenye vyombo vya habari kuwa awali Bana Ngenge ndiyo ilikuwa ikipiga Safari Resorts. Lakini walipokuja wao awali walidharaulika, lakini baadaye Bana Ngenge aliona moto ni mkali wakakimbia nchi.

Si wengi wanaojua kuwa kumbe Fredie Ndala Kasheba alikuwamo kwenye kikosi cha OSS Masantula Ngoma ya Mpwita ya Kiki kama mwanamuziki wa kawaida, akiwa na mkwe wakati huo, Bakambi Nkela ambaye naye alikuwa mwimbaji.

Wengi wanajua kuwa Kiki alipoondoka ndipo akaja Kasheba. Ukweli ni kwamba awali Kasheba alikuwapo kwenye kikosi cha kwanza, lakini kabla ya kurekodi akaondoka yeye na mkewe kwenda nchini Burundi kimuziki. Baada ya mkataba wa Kiki na OSS kumalizika, ndipo mmiliki wa bendi hiyo, Hugo Kisima, alipomrudisha Kasheba ambaye aliasisi mtindo wa Dukuduku.

Si mashabiki wengi pia wanaofahamu kuwa mwimbaji Lovy Longomba aliyewika nchini Kenya na Super Mazembe akaja nchini kujiunga na bendi ya African Sound 'Afriso Ngoma', ameshawahi kuimbia Maquiz Original na Bicco Stars kwa vipindi vifupi. Kabla ya kuingia Afriso alikuwa Maquiz, lakini alidakwa na mmiliki wa bendi hayati Juma Mwendapole na kumpeleka kwenye bendi yake.

Kabla ya kuunda bendi yake ya Super Lovy alipotoka Afriso, mwanamuziki huyo mwenye sauti nyororo alijiunga Bicco Stars alimfuata rafiki yake, Ramadhani Kinguti kwenye sauti nzito na alikuwa naye Afriso. Wengi hawajui habari hizo kwa sababu huko alikopitia hakurekodi.

Hata mpiga solo, Mosesengo Fanfan (sasa marehemu) ambaye wengi nchini wanajua alizipigia bendi ya Super Matimila na Orchestra Makassy, aliwahi kujiunga na Marquiz Original, lakini aliondoka kabla ya kurekodi, ndiyo maana wengi hawajui.

Leo nawapa hadithi ya bendi kongwe ya Dar Jazz ilivyotaka kupinduliwa na bendi yake ya kikosi cha pili.

Zamani bendi nyingi zilikuwa na vikosi vya pili kama timu za mpira wa miguu. Kikosi cha pili cha Dar Jazz kilipata mwanamuziki Patrick Balisidya. Hakuwamo kwenye kikosi cha kwanza kwa sababu kulikuwa na mkongwe Michael 'King' Enock ambaye alikuwa akipiga solo.

Balisidya alipiga solo na kuimba. Ilikuwa mwishoni mwa miaka ya 1960, Dar Jazz ilikuwa ikifanya onyesho kwenye ukumbi moja Dar es Salaam. Cha ajabu watu walikuwa wachache na si kawaida. Muda mfupi baadaye ikaja taarifa kuwa mashabiki wengi wa Dar Jazz wamefurika kwenye onyesho la Dar Jazz B. Hiyo ilimshtua King na mmiliki wa kundi hilo.

Kumbe Balisidya alipopelekwa kwenye kikosi cha pili, alitumia kipaji chake cha kupiga solo na kuimbaji kukibadilisha kikosi hicho na kuwa tishio si kwa Dar Jazz pekee, bali hata kwa bendi zingine.

King akamwambia mmiliki kuwa bila kuua bendi hiyo, Dar Jazz kubwa itapata shida sana kwa sababu mashabiki wameshatokea kuikubali na kupenda muziki wake. Ni kwa sababu bendi hiyo ilipiga miziki yenye staili zote za kisasa na kizamani. Ilipiga miziki ya kizungu kama ile ya kina James Brown, Kikongomani, mtindo kama ya Dar Jazz yenyewe kubwa, halafu wakatunga na kuimba nyimbo zao kisasa zaidi, hivyo kufanya mashabiki kuanza kuikacha bendi kubwa.

Mmiliki akavunja kikosi cha pili cha Dar Jazz. Wale wanamuziki walioonekana wakali, kama Balisidya na wengine wachache wakapandishwa kwenye kikosi cha kwanza. Hii ilimuuma sana Balisidya kwani alishaanza kutengeneza kama utawala wake hivi na umaarufu.

Kwa jinsi alivyoteka mashabiki, aliona ilikuwa ndiyo njia yake ya kutengeneza jina.

Hata hivyo ilimfunza kitu. Alijiona kumbe anaweza, hivyo lake lilikuwa rohoni.

Aliendelea kupiga Dar Jazz, lakini akiwa na sononeko moyoni hadi aliposaidiwa na baba yake mzazi kununua vyombo na kuunda bendi ya Afro Band, ambayo ilijulikana kama Afro 70 kutokana na kuundwa miaka hiyo na kujipatia umaarufu mkubwa.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-18

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALIPOANGALIA meseji zote zilitumwa siku ambayo yeye alikuwa amepoteza simu yake kimaajabu.

Aligundua pia meseji zile zilitumwa kuelekea kwenye namba ya marehemu mpenzi wake Tausi.

Alichogundua ni kwamba wizi wa simu yake ulifanyika kwa makusudi ili apoteze mawasiliano na mpenzi wake kwa ajili ya wao kuwasiliana naye kwa nia ya kumdanganya.

Baada ya hapo kwa mujibu za meseji zile ni kwamba baba yake alianza kumtumia meseji Tausi kwa namba yake msaada wa Doroth na kumlaghai kuwa anawasiliana na yeye Donald, kwa kumdanganya kuwa amepoteza simu kumbe sivyo.

Ulaghai huo ndiyo uliomfanya Tausi kudhani anaitwa Sinza, nia ilikuwa ni kwenda kumtoa uhai wake.


Hapo ndipo hata ule wasiwasi kuwa huenda aliitwa na mwanamume mwingine ulitoweka.

Kuanzia hapo hakuwa wa wasiwasi tena kama mpango mkakati wote wa mauaji, hadi kifo cha mpenzi wake kimefanywa na wazazi wake wote wawili, wakishirikiana na Doroth.

Akagundua siku ya tukio kulikuwa na mawasiliano kati ya baba yake na Doroth, pamoja na mtu mwingine ambaye hamfahamu kwa ajili ya kutekeleza mauaji, huku mama yake akitumika tu kumchukulia simu ili asiweze kuwasiliana na Tausi, kwa ajili ya kufanikisha mpango huo.

Aliangua kilio. Kilio cha kwikwi. "Baba na mama. Kwa nini mmefanya jambo hili? Jambo la kikatili. Mmemuua msichana wa watu. Mtoto masikini. Aliyekuwa akitegemewa na wazazi wake kwa ajili ya manufaa yenu?" Aliomboleza kana kwamba anamwambia mtu ndani ingawa alikuwa peke yake.

Ni kama vile msiba ulianza upya kwake. Alivuta picha kila kitu alichokuwa akifanya wakiwa pamoja. Upendo wa dhati waliokuwa nao. Ucheshi. Jinsi walivyokuwa wakitaniana. Wakila chakula pamoja. Wakilishana na kunyweshana. Donald alionekana kuchanganyikiwa. "Tausi umeniacha peke yangu. Hapa nimebaki na maadui watupu. Wauaji waliotoa roho yako. Lala pema mpenzi wangu. Nitahakikisha kila mmoja analipa hili alilolitekeleza kwako. Nakuahidi. Nakuahidi Tausi." Baada ya kumaliza kilio na maombolezo, usingizi mzito ukamchukua.




**Aliangua kilio. Kilio cha kwikwi. "Baba na mama. Kwa nini mmefanya jambo hili? Jambo la kikatili. Mmemuua msichana wa watu. Mtoto masikini. Aliyekuwa akitegemewa na wazazi wake kwa ajili ya manufaa yenu?" Aliomboleza kana kwamba anamwambia mtu ndani ingawa alikuwa peke yake.**

******************************

"Unaitwa nani?"

"Sadiki Mtumwa."

"Nimekuja hapa kutaka maelezo kidogo juu ya marehemu.

Siyo kama wewe unahusika, ila kusaidia kumhisi, au kutia mbaroni muuaji, sawa?"

"Sawa afande."

"Kwa hiyo usiwe na wasiwasi."

"Sawa."

Bado Sadiki alikuwa na wasiwasi. Alikuwa na mashaka kuwa anaweza kujibu maswali ambayo yanaweza kuonyesha kuwa rafiki yake Donald ndiyo muuaji. Hakutaka iwe hivyo. Lakini alijua kuwa Donald siyo aliyemuua Tausi.

"Nimeambiwa kwa miezi kadhaa, Tausi alikuwa akija nyumbani kwako. Ni kweli?"

"Ni kweli afande."

"Alikuwa mpenzi wako. Au?"

"Hapana."

"Alikuwa akifuata nini kwako?"

Alikuwa ni afande Peter aliyekuwa na cheo cha koplo. Alitumwa Inspekta Andrew kufanya upelelezi juu ya mauaji ya Tausi.

Inspekta Andrew alikaa na Koplo Peter kuangalia wanawezaje kumpata muuaji wa msichana huyo. Na kilichoamuliwa ni kuanza kazi hiyo nyumbani kwa marehemu.

Huko alikutana na wazazi na ndugu zake. Baada ya mahojiano ya muda mrefu, ilionekana kuwa marehemu kwa miezi kadhaa sasa alikuwa na urafiki mkubwa na Sadiki. Walijua sababu ya urafiki wao ni kwamba alikuwa na mpenzi aitwaye Donald.

Hawakutaka kumtaja kwa afande Peter kwa sababu hata wao walikua wa vyovyote iwavyo. Donald kwa jinsi alivyompenda ndugu yao, asingeweza kufanya hivyo.

Pamoja na misaada kadhaa ambayo alikuwa akiitoa moja kwa moja na mgine kupitia kwa ndugu yao, marehemu Tausi, dhamira iliwasuta.

Mzigo walimtupia rafiki yake Sadiki. Kama ni kumkaanga, basi huyo huyo ndiye afanye hivyo, lakini si wao.

"Mimi ni shemeji yake." Alijibu kwa ufupi.

"Shemeji yake kwa nani?"

"Rafiki yangu."

"Anaitwa nani?"

"Donald."

"Kwa nini awe anakuja hapa na siyo kwenda kwa Donald moja kwa moja?"

"Bwana afande kwa ufupi ni kwamba, rafiki yangu Donald anaishi kwa wazazi wake, ndiyo maana alikuwa hapendi kumpeleka kwao. Ndiyo maana alikuwa anamleta hapa. Hata alipompata alimpatia hapa kwangu." Sadiki alijibu akidhani tayari koplo Peter atakuwa ametosheka na majibu hayo.

Afande Peter mbali kuwa alikuwa akiandika kwenye kitabu kidogo, lakini pia alikuwa akirekodi kwenye simu ya mkononi. Yote hii ni kwa ajili ya ushahidi kama utahitajika mbele ya safari.

"Baada ya Tausi kufariki, rafiki yako alifika kwenye msiba?"

"Ndiyo afande. Na yeye ndiyo kwa kiasi kikubwa aligharamia msiba huo na tulikuwa naye siku zote za msiba hadi ulipomalizika."

"Inasemekana siku ya tukio aliondoka nyumbani kwao saa 12:00 jioni na mwili wake kukutwa kwenye mtaro pembeni mwa barabara Sinza, siku hiyo hukuwasiliana naye?"

Sadiki alifikiri kidogo. Alitaka kuongopa kuwa hakuwasiliana naye kabisa. Dhamira ikamsuta. Akaamua kujibu, ila kwa tahadhari kubwa.

"Aliniambia anatoka kidogo, ila hakuniambia anakwenda wapi." Aliongopa.

"Hakusema kama anakwenda kwa mpenzi wake?" Koplo Peter aliuliza kana kwamba alikuwa anajua Sadiki kwa jibu hilo amemuongopea.

"Hakukwambia kama anakwenda kwa mpenzi wake?"

"Hapana."

Ukweli hapa ni kwamba Tausi alimtaarifu Sadiki kuwa ametumiwa meseji na Donald wakutane mitaa ya Afrika Sana, Sinza.

Angethubutu tu kusema vile, basi rafiki yake angekuwa matatani. Ukweli aliopata baadaye ni kwamba wakati meseji hiyo ikitumwa, Donald alikuwa amepoteza simu yake. Kwa hiyo hapo kuna utata ambao hata yeye mwenyewe hauelewi. Na Donald alimthibitishia kuwa hakuwahi kumtumia meseji Tausi.

"Wewe unadhani kwamba alikwenda wapi?"

"Sijajua, yeye aliniambia anatoka kidogo. Angekwenda kwa Donald angeniambia. Unajia tena watoto wa

**INAENDELEA JUMAPILI**

# BURUDANI






## JITU BAYA ATAMBULISHA 'TWENDE NAO'

MWANAMUZIKI wa kufokafoka anayekuja kwa kasi, Jitu Baya, ametambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Twende nao' ambayo tayari inafanya vizuri.

Akizungumza na BT, Jitu Baya, ambaye anafananishwa na rapa mkongwe Chidi Benz, amesema ngoma hiyo inamtambulisha vizuri kwamba yeye si mtu wa maneno bali kazi.

"Ukitaka kupata mafanikio lazima kuachana na maneno ya watu, fanya kazi nzuri na kila mtu atakutambua na ndio maana nimewapa mashabiki wangu nyimbo hii kama zawadi yao ya kunivumilia," amesema.

Mwimbaji huyo wa FlowKali, amesema video ya wimbo huo ipo katika hatua ya mwisho kukamilika na wakati wowote itawekwa hadharani.

## Roma amtolea uvivu Nikki Mbishi



RAPA Roma Mkatoliki, ameamua kupasua jipu baada ya kumtaka Nikki Mbishi, kupunguza chuki dhidi ya wasanii wenzake.

Mwanamuziki huyo ambaye kwa sasa anaishi Marekani, amesema musiki si kusemana na kuwakasirikia watu wengine kwa sababu jambo hilo halijengi, bali linabomoa.

"Nikki punguza chuki, chuki zinamaliza kipaji chako, fanya muziki acha makasiriko kwa wasanii wenzako, acha chuki haikujengi inakubomoa kila leo" amesema Roma kupitia akaunti yake ya Instagram.

## LOVE JUAKALI JIKUBALI WEWE MREMBO

UKIDHANI unene wa kupitiliza si urembo, basi utakuwa umechelewa, kwani msanii wa filamu, Love Juakali, anajivunia kuwa na umbo hilo na mwili wake sawa na namba tisa.

Akizungumza na EATV, Love Juakali anasema hana haja ya kuongeza umbo kwa kuvaa kigodoro kwa sababu anajiamini na umbo lake na kwamba yeye ni mrembo.

"Kigodoro cha nini shepu yangu namba tisa inanitosha, ukiniambia nianze kuvaa kigodoro inaua muonekano wangu nataka kuwa hivi, Mungu hajataka nianze kuchonga sura au niwe mwembamba" amesema

Ameongeza "Mimi naamini kuwa natural, ujiamini na kuwa wewe, Watanzania wameumbiwa kuongea hawaridhikagi hata ukiwa na umbo".

HABARI MICHEZO




# KANE AKUBALI YAISHE, KUBAKIA TOTTENHAM

**LONDON,** England

KUELEKEA msimu mpya wa Ligi Kuu England wikiendi ijayo, nyota wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, ameamua kusema ya moyoni baada ya varangati la siku chache.

Kane aliweka wazi azma yake ya kutaka kuondoka Spurs kwenye dirisha hili la usajili, lakini mambo yamekuwa tofauti.

Kwa madai ya Kane, alikuwa na makubaliano ya mdomo kati yake na mmiliki wa Spurs, Daniel Levy, lakini amejikuta akiwekewa gharama kubwa kitu ambacho kinawashinda vigogo wa klabu zinazomtaka.


Kane aliende mbali zaidi kwa kutotokea mazoezini mapema wiki hii kama alivyotakiwa kufanya, kitendo hiki kiliibua hisia kwa mashabiki wa Spurs, wadau wa soka na vyombo mbalimbali vya habari kuhusisha tukio hilo na matakwa yake ya kutaka kuondoka.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Kane ameamua kuweka chapisho ambalo limeelezea kwa ufupi hisia zake kwa kile kinachoendelea.

Kati ya mengi aliyoandika, Kane amesisitiza kuwa hawezi na hana mpango wa kuvunja uhusiano wake na viongozi wa klabu, wachezaji wenzake na mashabiki ambao ndio watu muhimu zaidi kwenye maisha yake ya soka.

Kane ameongeza kuwa, atarejea mazoezini kama walivyokubaliana na kwamba ataendelea kucheza hapo.

Manchester City walikuwa wanahusishwa na kumtaka Kane, lakini sasa ndio basi tena.



## DYBALA, JUVENTUS WAJADILI MKATABA

**TURIN,** Italia

KWA mujibu wa vyanzo mbalimbali nchini Italia, wakala wa Paulo Dybala, Jorge Antun, jana alikutana na Juventus kwa ajili ya mazungumzo zaidi ya mkataba mpya wa mteja wake.

Antun aliwasili Italia akitokea Argentina wiki mbili zilizopita, lakini alilazimika kukaa karantini kwa takribani siku 10 kwa ajili ya kuendana na masharti ya Covid-19.

Kuna wasiwasi kuwa pande hizo mbili zinaweza kushindwa kufikia makubaliano katika mkutano wao wa kwanza.

Mkataba wa sasa wa nyota huyo wenye thamani ya euro milioni saba kwa mwaka, unaisha Juni mwakani.

Na Juventus wanatajwa kuwa wanataka kumpa mkataba mpya wa euro milioni nane pamoja na bonasi kufikia euro milioni 10.

Mkataba kama huu ulikataliwa mwaka uliopita, lakini Juventus wanaamini wanaweza kufikia makubaliano wakati huu kwenye dili hilo.

Zaidi, vyanzo vingine vinabainisha kuwa ikiwa pande hizi mbili zitashindwa kufikia muafaka basi zinaweza kukubaliana kuweka kipengele cha kumnunua kwa mkataba nyota huyo.

# PALMIERI CHAMBO KWA LUKAKU CHELSEA

**MILAN,** Italia

CHELSEA wanatajwa kuwa wanataka kujumuisha mabadilishano ya wachezaji kama sehemu ya dili la Romelu Lukaku, inadaiwa kuwa Emerson Palmieri ndiye anayefikiriwa kuwasilishwa kwenye ofa yao.

Taarifa zinaeleza kuwa klabu ya Inter Milan, wenyewe wanaweza kupokea fedha pekee na si mchezaji kama sehemu ya dili la Lukaku.

Chelsea wanaripotiwa kufikia ngazi ya makubaliano binafsi na mchezaji juu ya uwezekano wa nyota huyo kurejea Stamford Bridge akitarajia kupokea euro milioni 15 kwa msimu kwa miaka minne, pamoja na euro milioni tatu kwenye ada ya uhamisho.

Ofa yao ya hivi karibuni ya euro milioni 100 iliyomhusisha pia Marcos Alonso kama sehemu ya dili hilo ilikataliwa.

Vyanzo mbalimbali vinasisitiza kuwa Inter watakuwa tayari kupokea euro milioni 130 endapo ofa kama hii itawasilishwa.

Kutokana na kuongezeka kwa shinikizo kwa mashabiki, Inter Milan dili hili linaweza kuathirika kwa namna moja au nyingine, licha ya Chelsea kufanya jitihada za kuhakikisha wanakamilisha nia yao kabla ya mechi ya Uefa Super Cup dhidi ya Villarreal, Agosti 11 mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AHESABIWA SIKU KUJIFUNGA RASMI PSG

Pochettino ameviambia vyombo vya habari kuwa dili hilo linawezekana ndani ya...

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain inatajwa kuwa na uhakika wa kumsajili nyota, Lionel Messi, ndani ya wiki mbili na wakapata faida kwenye usajili huo.

Barcelona wamenyoosha mikono kuwa masharti ya mishahara ya LaLiga yamewashika shati, hivyo hawawezi tena kukamilisha kusaini mkataba mpya na Messi kama ilivyokuwa imekubaliwa awali na pande hizo mbili.

Kwa mujibu wa Sports Mole, baada ya Barca kutangaza kuwa hawawezi kumpa Messi mkataba mwingine, PSG tayari waliamua kufanya tathmini ya uwezekano wa kumsajili nyota huyo na pande zote za shilingi kwa faida na changamoto.

Tathmini ya ndani ya PSG inabainisha kuwa suala hilo linawezekana na linaweza kuwaongeza fedha kwa kuboresha udhamini na biashara kutokana na uwapo Messi.

Kocha Mauricio Pochettino, akizungumza na vyombo vya habari amebainisha kuwa dili la kumsaini Messi linawezekana na kwa sasa wanajaribu kufanya tathmini za msingi, amesisitiza kuwa klabu inafanya jitihada juu ya hilo.

PSG wana matumaini kuwa dili la Messi linaweza kuwalipa zaidi, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mauzo ya jezi.

## KWA UFUPI

### MOURINHO AMUWANIA DELANEY

KOCHA wa Klabu ya AS Roma, Jose Mourinho, yuko makini kumsajili mchezaji wa safu ya kati wa Borussia Dortmund, Thomas Delaney mwenye umri wa miaka 29, baada ya kushindwa kusaini mkataba na mchezaji wa kimataifa wa Uswisi, Granit Xhaka, 28, kutoka Arsenal. (Sun)

### ABRAMOVICH AJITOSA KWA MESSI

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich ameomba “mkutano wa dharura” na wawakilishi wa Lionel Messi baada ya kutangaza kwamba hataendelea tena na Barcelona. (AS)

### CHELSEA WAKOMAA NA LUKAKU

CHELSEA hawajakata tamaa ya matumaini ya kutia sahihi tena mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, kutoka klabu ya Serie A ya Inter Milan. (Athletic)

### RAMSEY AWANIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wameulizia juu ya uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Juventus na Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30. (Goal)

### NEYMAR AMVUTA MESSI

NYOTA wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, ametoa ofa ya kumpatia Lionel Messi jezi yake namba 10 kama atatua PSG. (RMC Sport via Get French Football News)

### HAALAND KUSUBIRIWA UTD

MANCHESTER United ina miezi 12 ya kumshawishi mshambuliaji wa Borussia Dortmund raia wa Norway, Erling Braut Haaland na kwamba ni klabu sahihi kwake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye anasakwa na Chelsea na klabu nyingine, anatarajiwa kuhama katika msimu wa majira ya joto wa mwaka 2022 wakati klabu zitakapoweza kutimiza kipengele cha kumuachia cha takriban pauni milioni 75 kwenye mkataba wake wa Dortmund. (Manchester Evening News)

### VILLA WARUDI KWA PROWSE

ASTON Villa wamewasilisha ofa ya pili kwa ajili ya kiungo wa kati wa Southampton, mwenye umri wa miaka 26, James Ward-Prowse baada ya ofa ya awali ya pauni milioni 25 kukataliwa. (Mail)

### ANSENSIO ATAKIWA EPL

KLABU za Leicester City, Leeds United na Everton zinashindana kuwania kumsaini winga wa Real Madrid Muhispania Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25. (Fichajes)

### TRIPPIER ANUKIA UNITED

ATLETICO Madrid wanajiandaa kwa uwezekano wa kumuuza mlinzi, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30 kwa klabu ya Manchester United ili kujiandaa kumchukua mchezaji wa Roma, Alessandro Florenzi, 30. (AS)

### VIEIRA AWANIWA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United ipo katika mazungumzo kwa ajili ya kuingia katika mkataba na kiungo wa kati wa kikosi cha zamani cha England cha vijana walio chini ya umri wa miaka 21, Ronaldo Vieira mwenye umri wa miaka 23, kutoka Sampdoria. (Mail)

### BOUBACAR HUYO NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanaangalia uwezekano wa kuingia mkataba na kiungo wa kati Mfaransa Boubacar Kamara mwenye umri wa miaka 21, kutoka Marseille kwa takriban pauni milioni 10. (Mail)

HABARI MICHEZO

# YANGA MAPEMA KUANZA KUJIWINDA MICHUANO CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya klabu ya Simba kutangaza kuwa inaanza rasmi mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mechi za kimataifa, klabu ya Yanga nayo imetangaza kuwa wachezaji wake wataanza kukusanyika na kuanza mazoezi, ikiwamo kuweka kambi rasmi kwa ajili ya msimu mpya, Agosti 15, mwaka huu.

Simba na Yanga zinakibarua cha kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani humu(CAF), huku Azam FC na Biashara United zikiwa na kibarua cha kuhakikisha bendera ya Tanzania inapepea vema katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Michuano hiyo inatarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza, lakini pia timu hizo vigogo nchini zinatarajiwa kufungua msimu wa ligi hiyo nchini Septemba 25, zikiwania Ngao ya Jamii.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said, amesema kuwa wataanza mazoezi Agosti 15 kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya ikiwamo michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hiyo ikiwa ni wiki moja baada mabingwa wa nchi, Simba inayotarajiwa kuanza kujifua leo.

"Tumesajili na tunaendelea kusajili kwa mapendekezo ya Kocha Mkuu wetu, Nabi (Nasreddine). Kuna baadhi ya wachezaji wameondoka kama vile Carlinhos (Carlos) kwa hiyo ni lazima tupate mbadala, lengo ni kuwa na kikosi bora," alisema.

Hersi, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM kwenye klabu ya Yanga, amewahakikishia wanachama na mashabiki kuwa usajili utafanywa kwa umakini zaidi.

Tayari klabu ya Yanga imewasajili wachezaji Fiston Mayele kutoka AS Vita ya DR Congo, Heritier Makambo ambaye amerejeshwa tena, akitokea Horoya alikokwenda akitokea klabuni hapo. Wote hao wakiwa ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Pamoja na hayo, Yanga inawachezesha kwenye michuano ya Kombe la Kagame baadhi ya wachezaji ambao inasemekana huenda ikawasajili, au imewasajili lakini bado haijawatangaza.

Wachezaji hao ni pamoja na kiungo matata wa Dodoma Jiji, Dickson Ambundo ambaye ameonekana kuvutia mashabiki wengi wa Yanga na Jimmy Ukonde mchezaji raia wa Msumbiji.

Yanga imeonekana kufanya usajili wa nguvu ikiwa na lengo la kutaka kurejesha heshima yake ya kutwaa mataji, kwani imekosa ubingwa wa Tanzania kwa misimu minne mfululizo ambayo watani zao, Simba imeubeba.

NIMEWASILI...



Yosso wa timu ya vijana ya Azam FC, Pascal Msindo (kushoto), akiwa na mwenyeji wake nchini Uturuki baada ya kuwasili salama jijini Antalya tayari kwa kuanza majaribio kesho ya kujiunga na timu ya Antalyaspor. **PICHA: MTANDAO**.

# Sonso mikononi tena kwa Mkwasa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ruvu Shooting umeendelea kujenga kikosi chao kwa kumnasa beki wa zamani wa Yanga, Ally Mtoni 'Sonso' kwa mkataba wa mwaka mmoja akitokea Kagera Sugar, alikokuwa akicheza msimu ulioisha wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Sonso alisema ameshamalizana na uongozi wa Ruvu Shooting kwa kusaini mkataba wa mwaka mmoja kutumikia kikosi hicho cha wajeda hao kwa msimu mpya wa ligi hiyo, inayotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Alisema mkataba na Kagera Sugar ulifikia ukingoni mwishoni mwa msimu na kutohitaji huduma yake, hivyo akaamua kuangalia 'nyasi' kwingineko kabla ya kupata malisho bora Ruvu Shooting na sasa ni mchezaji halali wa kikosi hicho.

"Ni kweli nimesaini mkataba wa mwaka mmoja na Ruvu Shooting baada ya pande zote kuelewana. Nina imani nitafanya vizuri kwa sababu ninauzoefu mkubwa wa ligi ya nyumbani, lakini kubwa ni kuhakikisha nashirikiana vizuri na wenzangu kufikia malengo ya timu," alisema Sonso.

Beki huyo wa kushoto anayemudu pia kucheza kama beki wa kati, amejiunga na Ruvu Shooting baada ya kuisaidia Kagera Sugar kusalia Ligi Kuu.

Aidha, imeelezwa beki huyo kutua kwake Ruvu shooting ni pendekezo la benchi la ufundi lililopo chini ya Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa, aliyewahi kufanya naye kazi wakati akiinoa Yanga.

Usajili huo wa Sonso ni wazi sasa anakwenda kurithi mikoba ya Charles Manyama aliyejiunga na Azam FC katika dirisha hili la usajili tayari kwa msimu mpya wa 2021/22.

# Azam kambini leo kusaka mbinu Ligi Kuu, kimataifa

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Azam FC, kinaingia kambini leo katika viunga vyake cha Chamazi, Dar es Salaam kwa muda wa siku 10 kabla ya baadaye kuihamishia kambi hiyo nje ya nchi kuendelea kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Azam itaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika ikibeba jukumu hilo pamoja na Biashara United katika michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu ikiwa ni siku 19 kabla ya Ligi Kuu Bara kuanza.

Azam ambao wamemaliza msimu katika nafasi ya pili nyuma ya Yanga na Simba, wamedhamiria kuvunja ufalme wa timu hizo kongwe wakati huu 'Wekundu wa Msimbazi' wakiwa wameubeba ubingwa huo mara nne mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wachezaji wanatakiwa kuripoti leo ili kuanza mazoezi rasmi kwa muda wa siku 10 na baadaye kwenda nje ya nchini.

Alisema wanatarajia kwenda nje ambapo watakuwa wakicheza mechi za kirafiki za ushindani ili kujiweka fiti kwa ajili ya michuano ya kimataifa ambayo itaanza kabla ya ligi.

"Ukizingatia ratiba imekuwa ngumu sana, tunaenda kucheza michuano ya kimataifa kabla ya kuanza kwa ligi, hivyo tunahitaji kupambana kupata mechi nyingi za kirafiki zilizokuwa na ushindani mkubwa kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu kuelekea michezo hiyo," alisema Popat.


Alisema ni mapema sana kuweka wazi kuhusu nchi watakayoweka kambi wakati huu wakihitaji kupata sehemu tulivua na mazingira rafiki kwa kocha George Lwandamina kuandaa kikosi chake.

Azam hadi sasa wamefanikiwa kufanya usajili wa wachezaji sita ambao ni Paul Katema, Roger Kolla, Edward Manyama, Charles Zulu, Idris Mbombo na mlinda mlango Salula kwa ajili ya michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajia kuanza kutimua vumbi Septemba 29.

# Michezo

Jumapili Agosti 8, 2021

Nipashe

Messi ahesabiwa siku kutua PSG

HABARI UK 22

## TFF kuteta na Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), linatarajia kukutana na wawakilishi wa nchi katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la mchezo huo Afrika (CAF), ili kuweka mikakati imara kuelekea msimu ujao wa michuano ya kimataifa.

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Yanga, Azam FC na Biashara United ndio watakaowakilisha nchi katika mashindano yajayo ya CAF yanayotarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu.

Akizungumza katika hotuba yake kwenye mkutano mkuu wa TFF, Rais Wallace Karia, ambaye jana aliidhinishwa kushika nafasi hiyo tena kwa kipindi cha miaka minne, alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha timu zote zinafanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho na hatimaye kulinda ushiriki wa klabu nne.

Karia alisema kuendelea kufanya vizuri mbali na kuongeza pointi kwa nchi, lakini pia kutaiweka kwenye nafasi bora ya kulitangaza zaidi jina la Tanzania kimataifa.

"Tutakaa vikao na wawakilishi wetu kujipanga kwa lengo la kufanya vema, nia yetu ni kuendelea kupata pointi nyingi na kuendelea kupata uwakilishi wa timu nyingi, si mpaka tusubiri timu za nchi nyingine zifanye vibaya," alisema Karia.

Kiongozi huyo alisema TFF pia inajipanga kuboresha miundo mbalimbali kuelekea msimu mpya, kwa kuendesha kozi endelevu kwa makocha na waamuzi wazalendo kwa ajili ya kuboresha viwango vyao.

Alisema pia malengo ya shirikisho ni kuona Timu ya Taifa (Taifa Stars) inapanda katika ubora wake hadi kuwa kwenye nafasi 20 bora kwa Afrika hadi kufikia mwakani sambamba na Timu ya Wanawake (Twiga Stars), kupanda hadi kuwa kwenye 10-bora ya Afrika.

Naye Mgeni rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, alisema: "Tanzania ni sehemu ya dunia, tunatakiwa kwenda sambamba, tunatakiwa kubadilika pamoja, niwapongeze hapa mlipofika mmeendelea sana, kuna mabadiliko makubwa sana, nilihudhuria mkutano wa uchaguzi mwaka 1996 pale Chuo Kikuu Dar es Salaam, mmepiga hatua njema."

YANGA 'OUT'...




Mshambuliaji wa Yanga, Waziri Junior (katikati), akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Express ya Uganda katika mechi ya Kombe Kagame iliyopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam jana na Yanga kuaga mashindano hayo baada ya kuangukia pua kwa mabao 3-1, hivyo kushika nafasi ya pili kutoka mkiani katika Kundi lao la B. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# NI KARIA, NYAMLANI TENA TFF

## ●●● Atema cheche akimpa ulaji mwanamke pekee aliyewania urais huku CAF, FIFA wakishuhudia...

**Na Somoe Ng'itu, TANGA**

WAKATI Wallace Karia akipita bila kupingwa katika nafasi ya urais kwenye uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), uliofanyika jijini Tanga jana, Lameck Nyambaya, ameshinda nafasi ya Ujumbe wa Kanda namba moja akimshinda Hosseah Lugano kwenye kanda hiyo.

Nyambaya ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), ameibuka mshindi baada ya kupata kura 40 wakati Lugano, Mwenyekiti wa FA Lindi akipata 35 na Mwenyekiti wa FA Mtwara, Athumani Kambi akiambulia kura 6.

Kanda namba mbili aliyeshinda ni Khalid Abdallah wa jijini hapa aliyepata kura 55 na mshindani wake Zakayo Mjema ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Arusha aliyepata kura 26 huku James Mhagama akiibuka mshindi katika Kanda namba tatu baada ya kupata kura 47 akifuatiwa na Abousufian Silia aliyepata kura 27 huku Mohammed Mashango akiambulia nane.

Mwenyekiti wa FA Dodoma (DOREFA), Mohammed Aden aliibuka kidedea katika Kanda namba nne baada ya kupata kura 53 na kuwashinda Osuri Kosuri aliyepata kura 20 na Hamisi Kitila aliyepata kura nane.

Mshindi wa Kanda namba tano ni Vedastus Lufano aliyepata kura 35 akiwashinda Salum Chama aliyepata kura 32 na Salum Kulunge aliyeambulia kura 14 huku Issa Bukuku kutoka mkoani Kigoma aking'ara katika Kanda namba sita.

**Bukuku, Katibu Mkuu wa zamani wa Chama cha Soka Mkoa wa Kigoma (KFA), alipata kura 58 wakati wapinzani wake Blassy Kiondo na Kenneth Pesambili kila mmoja alipata kura 11.**

Kwa mujibu wa Katiba ya TFF, Karia alitangaza wajumbe wanne wa kuteuliwa ambao ni Athumani Nyamlani, Ahmed Mgoyi, Saidi Soud na Hawa Mniga, aliyekuwa mgombea pekee mwanamke katika nafasi ya urais katika uchaguzi huo, lakini aliondolewa kwa kutokidhi sifa.

Karia pia alimteua Nyamlani kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa shirikisho hilo, na wajumbe wa mkutano mkuu walimthibitisha.

Pia kiongozi huyo aliwashukuru wajumbe wa mkutano mkuu kwa kuwarejesha madarakani na kuwapa heshima ya kuwaongoza kwa muda mwingine kama katiba inavyoelekeza.

Aliwataka wagombea ambao kura zao hazijatosha, kuungana nao kufanya kazi za mpira na kamwe wasiparaganyike.

"Nyinyi wote ni wangu, na bahati nzuri wengi wenu ni wenyeviti wa mikoa, ni vizuri twende tukaufanyie kazi mpira, mnachezesha ligi ambazo hazileti tija, waambieni wabunge hayo mashindano yao yawe katika kalenda," Karia alisema.

Alisema pia kutakuwa na Tuzo ya Mwenyekiti Bora wa mkoa anayefanya vizuri na mshindi atapata Sh. milioni 10 ambazo zitakwenda kuendeleza programu za maendeleo na kuwatambua kwa mazuri yao wanayofanya, lakini pia akisisitiza ushirikiano.

Aliongeza kuwa shirikisho hilo litakuwa na mabadiliko mbalimbali yenye lengo la kufikia mafanikio, lakini akiwakumbusha viongozi wa mikoa kushirikiana na viongozi wa serikali za mikoa na kuacha vurugu ambazo hazina afya na zitakazomaliza migogoro.

"Niwaambie nawashukuru, hatutawaangusha, tusipoenda sawa sawa huko mbele tutaburuzana," Karia alimaliza.

Uchaguzi huo ambao viongozi wake watakaa madarakani kwa muda wa miaka minne, ulisimamiwa na kushudhuriwa na waangalizi kutoka katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na FIFA.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042